# MATUMIZI YA TARAKILISHI KATIKA UFUNDISHAJI WA FASIHI SIMULIZI KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA: UCHUNGUZI KIFANI WA KAUNTI YA BUNGOMA

**Kibiti David Barasa**

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Elimu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kibabii

MEI 2018

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO LA MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kingine chochote.

**Kibiti David Barasa**

**MED/KIS/006/2014**

Sahihi …………………………………… Tarehe …………………………………….

### IDHINI YA WATAHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo.

**Dkt. Fred Wanjala Simiyu,**

Sahihi ……………………………………Tarehe ……………………........................

Idara ya Kiswahili na Lugha zingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Kibabii.

**Dkt. Ben Nyongesa,**

Sahihi ……………………………………Tarehe ……………………........................

Idara ya Kiingereza, Fasihi na Mawasiliano,

Chuo Kikuu cha Kibabii.

## IKIRARI NA HATIMILIKI

Mimi, David Kibiti Barasa, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe, haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya shahada kama hii au nyingine yoyote. Tasnifu hii ya Shahada ya uzamili ya Kiswahili ni kazi inayolindwa kwa mujibu wa makubaliano ya mswada wa kisheria wa Berne, kifungu cha hati miliki cha mwaka 1999 na sheria nyingine za kitaifa na kimataifa, kwa niaba ya mwanataaluma. Kazi hii hairuhusiwi kutolewa kwa namna yoyote ile, yote au sehemu, isipokuwa kwa matumizi ya kitaaluma ya utafiti, kujisomea na kurejelea kwa kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Masomo ya Uzamili kwa niaba ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya.

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mke wangu mpendwa Catherine Kibiti, binti yangu Belinda Kibiti pamoja na marehemu mwanangu Mitch Kibiti kwa uaminifu na msaada wao wa dhati.

# SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika umbali huu. Nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Fred S. Wanjala na Dkt. Ben Nyongesa kwa kujitolea kuniongoza katika safari hii ndefu. Nawaombea baraka ili wawe wa manufaa kwa wengine. Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wote walionielekeza masomoni. Ningependa kuwashukuru Dkt. Carren Nyandiba (Chuo Kikuu cha Rongo), Dkt. Deborrah Amukowa (Chuo Kikuu cha Maseno), Dkt. Nilson Opande (Chuo Kikuu cha Kisii) na Mwalimu Eric Wamalwa (Chuo Kikuu cha Kibabii) kwa mchango wao mkubwa. Nashukuru Chuo Kikuu cha Kibabii kwa kunipa nafasi ya kuongeza masomo yangu. Isitoshe, ningependa kuwashukuru wenzangu Martin Luta, Rose Abai, Anne Nabutola, Stephen Ndinyo na Hillary Mauka kwa kunitia moyo kila wakati. Shukrani tele kwa jamaa zangu, Prof. Donald Siamba, Dkt. Rispa Wepukhulu, ndugu na dada zangu pamoja na wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine. Shukrani za mwisho ziiendee familia yangu kwa uvumilivu na kunitia moyo katika safari hii. Mungu awazidishie neema na uwezo. Kwenu nyote nasema Mungu awabariki sana.

# IKISIRI

Matumizi ya teknolojia za kisasa katika mawasiliano ni muhimu sana leo. Katika muktadha wa elimu, mbinu za kurahisisha mawasiliano darasani ni muhimu ili kuhakikisha matokeo mema katika mtihani na pia kuwaandaa wanafunzi katika matumizi ya vifaa vya kisasa wanapomaliza shule. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu matumizi ya tarakilishi katika shughuli za elimu lakini hapana wowote tulioshuhudia unaohusu ufunzaji wa Fasihi Simulizi kwa kutumia tarakilishi. Pengo hili ndilo ambalo limejenga msingi wa utafiti huu. Basi katika utafiti huu, Mtafiti alichunguza matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi. Utafiti huu hasa ulilenga kutathmini ni kwa kiwango kipi walimu wa Kiswahili hutumia tarakilishi katika kufunza Fasihi Simulizi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Ukubalifu na Utumizi wa Teknolojia iliyoasisiwa na Rogers (2003). Nadharia hii inafafanua hatua wanazopitia watumizi kabla ya kuanza kutumia teknolojia mpya katika shughuli zao. Utafiti uliegemea muundo wa kithamano na mkabala wa usoroveya na ulifanywa katika shule teule za upili katika kaunti ya Bungoma. Sampuli ya shule 18 iliteuliwa katika jumla ya shule teule za kaunti ndogo katika kaunti nzima. Shule hizi zimepandishwa vyeo mwaka wa 2010 na kufanywa kuwa shule teule katika kila eneo bunge. Wasailiwa walipatikana kutoka kwa jumla ya shule 314 za kaunti ya Bungoma. Sampuli ilijumlisha walimu wa Kiswahili 36, walimu wakuu 18 wa shule zilizoteuliwa. Jumla ya watafiti walikuwa 54. Mbinu za kuteua sampuli zilikuwa sampuli maksudi, sampuli nasibu tabakishi na sampuli nasibu. Utafiti huu ulitumia hojaji na mahojiano kama mbinu za kukusanya data. Hatimaye, data hizo zikawasilishwa na kuchanganuliwa kwa majedwali, nambari na asilimia. Mtafiti alipata kwamba shule zote kati ya zilizoteuliwa zina tarakilishi. Hata hivyo, hizi tarakilishi hazikutumiwa na walimu katika shughuli za kufunza darasani. Pia, ilibainika kuwa kuna changamoto zinazoathiri matumizi ya tarakilishi kama wenzo wa kufunzia. Mfano mwema ni ukosefu wa ujuzi wa tarakilishi miongoni mwa walimu na umeme usiotegemewa. Inatarajiwa kwamba matokeo yatawasaidia walimu kuboresha mbinu za ufunzaji hasa wa Fasihi Simulizi kwa kutumia teknolojia za kisasa. Serikali na wadau katika elimu watayaboresha mazingira ya elimu.

## ABSTRACT

The use of modern technological tools in communication has been a subject of interest lately. In the field of education, the use of modern tools to improve learning outcomes is no longer optional, because it improves the learning environment and prepares the learner to fit in the technological age after school. Much research has been done on the use of computers in education but so far none has been done to specifically examine how computers are used to teach oral literature in Kiswahili. Therefore the main purpose of this research was to find out how teachers use computers to teach oral literature in Kiswahili in schools in Bungoma County. It was this gap that prompted this research to be carried out. The research was carried out in the newly created schools of excellence (Centres of Excellence) in Bungoma county. The research used survey method and was guided by the Technology Adoption and Diffusion theory of Rogers (2003). This theory outlines the steps users go through before they finally accept and start to use new technology. Participants were drawn from a population of 314 secondary schools in Bungoma county. These schools were recently upgraded and made to be schools of excellence in every constituency. The total number of respondents was 54 from those Centres of Excellence who included 18 head teachers and 36 Kiswahili teachers. Purposive, random and simple stratified sampling methods were used to select the respondents. Instruments of data collection used were questionnaire and interview methods. The findings were analysed and presented by use of tables, percentages and explanations. The researcher found out that while all schools had computers either in offices or in computer rooms, little effort was applied to use them in teaching of oral literature. It was also revealed that there are several challenges that have hampered the use of computers in teaching oral literature in secondary schools, e.g lack of computer skills among teachers and power shortages. It is hoped that the findings of the study will help teachers of oral literature to improve their teaching techniques by employing newer forms of technology like the use of computers. The government and stakeholders in education will be sensitized on the value of instructional resources and therefore avail them in schools.

## YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI ...... i**

**IKIRARI NA HATIMILIKI ...... iii**

**TABARUKU ...... iv**

**SHUKRANI...... v**

**IKISIRI...... vi**

**ABSTRACT ...... vii**

**YALIYOMO ...... viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI ...... i**

**ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU ...... xiv**

**FASILI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIWA...... xvi**

**SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI...... 1**

1.1 Utangulizi ……..i

1.2 Usuli wa mada……1

1.3 Suala la utafiti…….5

1.4 Malengo ya utafiti……6

1.5 Maswali ya utafiti ……..7

1.6 Umuhimu wa utafiti huu…….8

1.7 Upeo na mipaka ya utafiti……..8

1.8 Misingi ya nadharia……..10

1.9 Muhtasari……..12

**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI ...... 13**

2.1 Utangulizi ……13

2.2 Dhana ya tarakilishi……..13

2.3 Dhana ya Fasihi Simulizi……………………………………………………………….14

2.4 Matumizi ya vifaa vya kufunzia……………………………………………….…..15

2.5 Matumizi ya tarakilishi darasani…………………………………………….……….16

2.6 Matumizi ya tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi……………………………………19

2.7 Muhtasari …………………………………………………………………………23

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ...................................................................... 24**

3.1 Utangulizi…………………………………………………………………………….24

3.2 Muundo wa utafiti……………………………………………………………………24

3.3 Eneo la utafiti………………………………………………………………………...25

3.4 Wasailiwa lengwa ……………………………………………………………………26

3.5 Sampuli na usampulishaji…………………………………………………………….27

3.5.1 Sampuli kusudio……………………………………………………………………28

3.5.2 Usampulishaji nasibu tabakishi…………………………………………………….28

3.5.3 Usampulishaji nasibu…………………………………………………………...29

3.6 Mbinu za kukusanya data ……………………………………………………………29

3.6.1 Hojaji……………………………………………………………………………….29

3.6.2 Mahojiano…………………………………………………………………………..30

3.7 Uhalali na ubora wa vifaa vya utafiti………………………………………………...30

3.7.1 Utafiti wa awali ……………………………………………………………………31

3.7.2 Uhalali wa matokeo………………………………………………………………...31

3.7.3 Utegemezi wa vifaa………………………………………………………………...32

3.8 Uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo……………………………………32

3.9 Changamoto za utafiti………………………………………………………………..33

3.10 Maadili ya kitafiti…………………………………………………………………...34

3.11 Muhtasari……………………………………………………………………………34

**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA ........................................................ 35**

4.1 Utangulizi……………………………………………………………………….35

4.2 Viwango vya matumizi ya tarakilishi katika kufundishia Fasihi Simulizi…………...35

4.3 Maandalizi ya vipindi vya Fasihi Simulizi kwa kushirikisha tarakilishi……………..46

4.3.1 Maazimio ya kazi……………………………………………………………..46

4.3.2 Mpangilio wa somo…………………………………………………………...47

4.3.3 Nukuu za masomo……………………………………………………………48

4.3.4 Maandalizi ya wanafunzi na walimu wasaidizi ……………………………………49

4.4 Changamoto katika matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi…....51

4.4.1 Uhaba wa tarakilishi…………………………………………………………..51

4.4.2 Ufupi wa wakati………………………………………………………………52

4.4.3 Ukosefu wa ujuzi wa kutumia tarakilishi……………………………………..54

4.4.4 Matatizo ya umeme…………………………………………………………...56

4.4.5 Ukosefu wa mada za Fasihi Simulizi…………………………………………56

4.4.6 Fikra za kutosheleka kwa walimu…………………………………………….57

4.5 Mbinu mbadala wanazotumia walimu kufunzia Fasihi Simulizi……………………58

4.5.1 Maoni ya wasailiwa…………………………………………………………...59

4.5.2 Mbinu ya kuuliza na kujibu maswali…………………………………………59

4.5.3 Mbinu ya Maelezo……………………………..……………………………60

4.5.4 Majadiliano……………………………………………………………………61

4.5.5 Kanda na santuri………………………………………………………………61

4.5.6 Mbinu ya maigizo……………………………………………………………..62

4.5.7 Mbinu ya mhadhara…………………………………………………………...62

4.5.8 Mbinu ya wageni waalikwa…………………………………………………...63

4.5.9 Kazi mradi…………………………………………………………………….64

4.5.10 Mbinu ya ziara …………………………………………………………………64

4.6 Hitimisho ……………………………………………………………………65

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................ 66**

5.1 Utangulizi ……………………………………………………………………66

5.2 Muhtasari wa tasnifu…………………………………………………………66

5.2.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti…………………………………………...67

5.2.2 Viwango ambavyo walimu hutumia tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi…………68

5.2.3 Tarakilishi katika maandalizi na ufunzaji wa Fasihi Simulizi……………………..68

5.2.4 Changamoto za kutumia tarakilishi……………………………………..69

5.2.5 Mbinu wanazotumia walimu kufunzia Fasihi Simulizi ……………………………70

5.3 Hitimisho…………………………………………………………………..70

5.4 Mapendekezo…………………………………………………………………70

5.5 Mapendekezo kwa tafiti za baadaye…………………………………………72

**MAREJELEO………………………………………………………………..……74**

**VIAMBATISHO…………………………………………………………...…81**

Kiambatisho 1: Hojaji ya walimu wa Kiswahili............................................................ 81

Kiambatisho 2: Hojaji ya walimu (Mfano wa nakala iliyojazwa)................................... 83

Kiambatisho 3: Mahojiano na walimu.................................................................... 85

Kiambatisho 4: Mahojiano na walimu (Mfano wa nakala iliyojazwa) ............................ 87

Kiambatisho 5: Hojaji ya walimu wakuu ...................................................................... 88

Kiambatisho 6: Hojaji ya walimu wakuu (Mfano wa nakala iliyojazwa)........................ 90

Kiambatisho 7: Utazamaji wa kipindi ........................................................................... 92

Kiambatisho 8: Utazamaji wa kipindi (Mfano wa nakala iliyojazwa) ............................. 93

Kiambatisho 9: Mfano wa azimio la kazi....................................................................... 94

Kiambatisho 10: Mbinu za kufundishia miongoni mwa walimu ..................................... 96

Kiambatisho 11: Ramani ya kaunti ya Bungoma .............................................................. 97

Kiambatisho 12: Barua ya idhini kutoka SGS................................................................... 98

Kiambatisho 13: Barua ya idhini kutoka NACOSTI......................................................... 99

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 4.1: Tarakilishi zitumikazo na zilizoharibika shuleni………… 36

Jedwali 4.2: Matumizi ya tarakilishi kufunzia………………………… 39

Jedwali 4.3 Namna walimu hutumia tarakilishi darasani……………… 40

Jedwali 4.4 Namna walimu walipata ujuzi wa tarakilishi……………… 41

Jedwali 4.5 linaonyesha namna tarakilishi kutumia tarakilishi………… 42

Jedwali 4.6 Vipengele vilivyofunzwa kwa kutumia tarakilishi………… 42

Jedwali 4.7 Idadi ya walimu waliotumia tarakilishi kuandaa nukuu…… 48

Jedwali 4.8 Changamoto katika harakati za kutumia tarakilishi……….. 51

Jedwali 4.9 Mbinu za kufundishia ambazo walimu hutumia shuleni….. 59

## ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| BAMIKE | Baraza la Mitihani Kenya |
| BKSUT | Baraza la Kitaifa la Sayansi Uvumbuzi na Teknolojia |
| CDE | *County Director of Education* |
| DEO | *District Education Office* |
| HOWA | Hojaji ya Mwalimu |
| HOWAWA | Hojaji ya Walimu Wakuu |
| KCSE | *Kenya Certificate of Secondary Education* |
| Khj | Keshatajwa |
| KICD | *Kenya Institute of Curriculum Development* |
| KIE | *Kenya Institute of Education* |
| Kv | Kama vile |
| MAWA | Mahojiano ya Walimu |
| MAWAWA | Mahojiano ya Walimu Wakuu |
| MOE | Ministry of Education |
| NEPAD | *New Partnership for Africa's Development* |
| Nk | Na kadhalika |
| NUMT | Nadharia ya Ukubalifu na Matumizi ya Teknolojia |
| SSJ | Shule ya Shahada za Juu |
| TENK | Taasisi ya Elimu Nchini Kenya (KIE) |

| | |
|---|---|
| TUMK | Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) |

## FASILI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIWA

| | |
|---|---|
| *Google* | Programu maalumu inayowezesha habari yoyote kutafutwa katika tovuti. |
| *Kakapel* | Mapango katika sehemu ya Teso, katika kaunti ya Bungoma, ambako inaaminika kwamba tohara ya Wabukusu ilianzia na hivi sasa ni mojawapo ya hifadhi ya taifa nchini Kenya. |
| *Khulicha* | Matambiko maalum ya baada ya tohara na ambayo yana usiri mwingi katika jamii ya Watachoni na baadhi ya koo za Wabukusu. |
| *Khuminya* | Sherehe maalumu za tohara katika jamii ya Wabukusu. |
| Kikokotozi | Kifaa cha kuchanganua hesabu. |
| Kinuruweo | Kifaa cha kuonyesha picha na maandishi ukutani kutoka kwenye tarakilishi (Projekta) |
| Kupakuliwa | Utoaji wa habari kutoka katika mtandao. |
| *Matuko Weye* | Mhusika katika riwaya ya Ken Walibora ya *Kidagaa Kimemwozea*. |
| *Mangulieche* | Mzee aliyekuwa na ufahamu mkubwa wa mila na desturi za Wabukusu na ambaye kwa ustadi mkubwa aliendesha shughuli za matambiko baada ya watu mashuhuri ama wazee kuaga dunia. |
| Mchakato | Namna fulani ya mfuatano wa mambo yaliyopangiliwa kufanyika katika utaratibu maalumu ili kutimiza mipango iliyowekwa. |
| Mitihani ya kushtukiza | Mitihani isiyopangiwa muda maalumu na ambayo huletwa wakati wowote. |
| Tovuti | Mahali katika mtandao palipo na ukurasa mmoja ama zaidi zinazoweza kutoa taarifa fulani kuhusu jambo katika mtandao. |

| | |
|---|---|
| *Yahoo!* | Mtandao wa kijamii unaotumiwa kutuma na kupokea nyaraka mbalimbali pamoja na kutafuta habari zozote. |

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Katika sura hii Mtafiti alijadili usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, lengo la utafiti, na umuhimu wa utafiti  huu. Kadhalika sura hii iliangazia upeo na mipaka ya utafiti pamoja na misingi ya nadharia iliyouongoza utafiti.

## 1.2 Usuli wa mada

Kiswahili ni mojawapo ya masomo yanayofunzwa katika shule za upili nchini Kenya. Odeo (2003) anasema kwamba asilimia themanini (80%) ya Wakenya huzungumza Kiswahili.  naye Muindi (2008) anadai kuwa katika eneo la Afrika Mashariki, Kiswahili kinachukuliwa kama lugha inayoweza kuleta uwiano na kuimarisha uchumi wa mataifa husika. Katiba ya Jamhuri ya Kenya (2010) imetambua Kiswahili kama lugha rasmi na pia lugha ya taifa.

Kwa mujibu wa ya Ripoti ya Koech (1999) Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili na hutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne. Katika mabadiliko ya mtaala yaliyofanywa mwaka wa 2002 na Taasisi ya Elimu Nchini Kenya (TENK) somo la Kiswahili liliongezewa vipengee kama vile Fasihi Simulizi, isimu-jamii na hadithi fupi. Mabadiliko haya yalilazimu kwamba walimu waboreshe mbinu za ufunzaji ili wanafunzi wapate matokeo mema katika somo la Kiswahili. Mbinu mwafaka za ufunzaji zimejikita katika uvumbuzi wa teknolojia.

Teknolojia imejipenyeza katika sekta mbalimbali na kubadili matokeo kazini. Kwa mfano, sasa tarakilishi hutumiwa katika sekta za afya, benki, biashara, ufundi viwandani, usafiri, utawala pamoja na elimu. Ni jambo la lazima kuwa tarakilishi itumiwe kwa shughuli za elimu kwa sababu ya manufaa yake. Serikali iko mstari wa mbele kwa kuzingatia mfumo wa utawala wa dijitali (*e-government*) ulioanzishwa mwaka 2004 lakini umeshika kasi miaka miwili iliyopita. Mengi ya mawasiliano na shughuli za serikali aghalabu hufanywa sasa kwa mfumo wa dijitali.

Ni jambo la busara kwamba sekta ya elimu pia izingatie mfumo huu wa dijitali. Walimu na wanafunzi watapata faida chungu nzima kutokana na matumizi ya tarakilishi. Mbinu tofauti za ufunzaji huwa na matokeo ya viwango tofauti Patel na Mukwa (1993). Waandishi hawa wanatilia mkazo kwamba walimu wazingatie mbinu za kuona, kusikiliza na kutenda ili kuteka akili za wanafunzi wao na pia kuleta uhai darasani. Mtaala wa elimu unasisitiza matumizi ya vifaa tofauti katika ufunzaji ili kuwasisimua wanafunzi na kuwasaidia kukumbuka waliyosoma TENK (k.h.j).

Teknolojia ni kigezo muhimu katika elimu. Murray na Waller (2007) wanasema kuwa matumizi ya teknolojia katika ufunzaji yanawezesha shughuli za kielimu kufanyika wakati wowote na mahali popote. Tarakilishi inafanya kazi kwa wepesi wa hali ya juu, yaani ndani ya sekunde chache mtu anaweza kupata ujumbe wowote anaotaka. Hesabu ngumu zinaweza kufanywa katika muda mchache kuliko unapotumia vifaa vingine kama vile kikokotozi ama kwa ujuzi wa ubongo wa binadamu. Wanafunzi na walimu wanaweza kupata ujumbe kwa urahisi kutoka kwa mitandao, na hata kushirikiana na wenzao walio katika sehemu tofauti za dunia. Johnson (2007) anadai kuwa manufaa ya

teknolojia katika elimu yanaelekea kushawishi watafiti wengi na hata washikadau kuwa litakuwa jambo la busara teknolojia tofauti zikitumiwa zaidi katika shughuli za elimu. Wanafunzi wanaweza kuuliza maswali na kujibiwa moja kwa moja, haraka na kwa njia tofauti. Pia, tarakilishi inaweza kutumiwa kufanya majadiliano ya kielimu yanayohusu urushaji na upokeaji wa habari kati ya wataalamu walio karibu na mbali.

Uvumbuzi wa tarakilishi umebadili pakubwa njia za mawasiliano na namna ya kufanya kazi. Tarakilishi au kompyuta ni aina ya mashine inayopokea habari na kuzishughulikia kulingana na programu inayopewa. Kifaa hiki hufwata hatua na mantiki katika utendaji kazi wake. Derek (2003) anaelezea tarakilishi kama aina ya teknolojia iliyo na uwezo wa kupokea ujumbe, kuchanganua, kuuweka na hata kusambaza kwa haraka sana. Kifaa hiki kina kisaidizi na programu ndani mwake inayoelekeza jinsi ya kufanya kazi kwa ukamilifu. Inafanya kazi kwa ubora bila makosa na ikiwa kosa linatokea itaonyesha ili urekebishe.

Tarakilishi na simu za rununu zimetumiwa katika nchi zilizoendelea kuimarisha elimu. Robertson (2000) anasema kwa wanafunzi hupata fursa ya kuchagua wanachotaka kusoma, kufanya utafiti wenyewe, kuwasiliana na hata kujitathmini. Tarakilishi huwezesha kutafuta vipengele muhimu vya masomo mbalimbali kwa mtandao na kupata ujumbe kwa muda mfupi kuliko vile ungetumia marejeo yaliyochapishwa.

Alonso (2005) anasema kuwa tarakilishi ina uwezo mkubwa wa kuhifadhi ujumbe kisha ukarejelewa baadaye. Watafiti wengi hutegemea tarakilishi kupata ujumbe uliohifadhiwa kwenye mtandao. Picha za mazingira tofauti na tamaduni zinaweza kupatikana katika

tarakilishi. Hivyo basi walimu wanaweza kutumia tarakilishi kuandaa vipindi vya elimu katika masomo tofauti shuleni na vyuoni.

Walimu wanaweza kutumia tarakilishi kubadilishana maoni na walimu wenzao, wanafunzi walio mbali, kutafiti mada, kuboresha mazingira darasani na hata kutahini wanafunzi. Walimu wanaweza kuandaa na kuonyesha picha kwa kutumia tarakilishi na projekta ili kuonyesha mada zinazofundishwa. Geer na Sweeny (2012) walidai kuwa tarakilishi ina uwezo wa kunasa akili za wanafunzi na kupanua fikra zao. Tarakilishi zina programu maalum kama picha, michoro na ramani, vitu ambavyo vinaweza kutumiwa kufunzia vipengele vya Fasihi Simulizi kama vile ngano, nyimbo, semi na maonyesho ya sanaa.

Matumizi ya tarakilishi yanaweza kuboresha matokeo ya wanafunzi katika mitihani. Wao wanaweza kupata ujumbe kwa urahisi, kufanya utafiti mwingi, kupata na kuchuja habari kulingana na mada wanazorejelea. Pia, maarifa na ujuzi wanaopata wanafunzi kutokana na tarakilishi ni maandalizi mazuri kwao kukabiliana na changamoto tofauti mahala pa kazi. Wanapotumia tarakilishi katika masomo wanapata ujuzi na mazoea ya kutumia vifaa hivi baadaye wanapoajiriwa. Katika ulimwengu wa sasa, ujuzi wa kutumia tarakilishi ni kipengele cha lazima kabla mtu kuajiriwa katika maeneo mengi ya kazi. Hii ni kwa sababu tarakilishi ndizo zinazotumiwa katika uendeshaji wa shughuli anuai katika sekta hizo.

Upungufu wa walimu ni tatizo kubwa hasa ikichukuliwa kuwa serikali ya Kenya imepunguza gharama ya elimu kwa wanafunzi katika shule za msingi na za upili kuanzia mwaka 2002. Idadi ya wanafunzi madarasani imeongezeka kufikia hata

wanafunzi mia moja kwa mwalimu mmoja katika shule za msingi za umma. Ikiwa kuna tarakilishi, mwalimu anaweza kuitumia kufunza wanafunzi wengi wakati mmoja.

Matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji katika nchi zinazoendelea bado ni changa. Nchini Kenya, serikali imepiga hatua kwa kutoa tarakilishi kwa shule na hata kuandaa mafunzo kwa walimu ili waweze kutumia tarakilishi katika kufunza. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (TUMK) imeandaa mada katika muundo wa dijitali kufunzwa katika shule za msingi. Pia serikali imo katika harakati za kutoa nguvu za umeme katika kila shule ili vifaa vya kiteknolojia viweze kutumiwa katika ufunzaji. Juhudi hizi zote zinafaa. Serikali inajitahidi kuhakikisha kuwa wanafunzi wengi zaidi wanapata elimu ya hali ya juu ili kutimiza malengo ya Ruwaza ya Mwaka 2030. Kwa vile matumizi ya tarakilishi yameshika kasi katika sekta mbalimbali, utafiti huu umeandaliwa ili kuchunguza ikiwa walimu hutumia tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi.

**1.3 Suala la utafiti**

Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ni suala ambalo limeangazwa kwa muda sasa na walimu katika kizazi cha leo. Sababu kuu ni kwamba kumetokea mabadiliko mengi katika uwasilishwaji wake. Awali amali za Fasihi Simulizi zilifundishwa na mafanani kama vile mababu, mashangazi, wajomba na wazee wenye umri mpevu. Magwiji hawa wa zamani wamezidi kudidimia kila kukicha kufuatana na vifo vyao pamoja na mabadiliko yanayotokea kila siku duniani. Leo hii maisha yamekumbwa na usasa unaotokana na kuzuka na kukita mizizi kwa masomo na teknolojia ngeni. Mabadiliko haya yameshuhudiwa katika kila upembe wa dunia hii. Katika kitengo cha elimu, mabadiliko haya yameshuhudiwa hadi katika ufundishaji wa vipengele vya Fasihi Simulizi. Mbinu za

zamani za kufundishia Fasihi Simulizi kama masimulizi, maelezo, mialiko ya mafanani shuleni ama kuwatembelea nyanjani imetumiwa kwa muda mrefu. Hata hivyo, matumizi haya yanaonekana yakiendelea kupoteza nguvu zake hivi sasa. Mabadiliko haya yamekuwa muhimu katika kuzua haja ya kutalii na kutambua mbinu zingine ambazo zinaweza kutumiwa kuboresha ufundishaji wa somo hili katika karne ya ishirini na moja. Mbinu mojawapo na ambayo ni ya muhimu ni matumizi ya tarakilishi.

Fasihi Simulizi inaweza kuwa tata katika ufundishaji wake kwa sababu ya maisha ya usasa ambapo wengi wa walimu na wanafunzi wamelelewa nje ya mazingira ya desturi zao za kiasili. Mazingira hayo yalisheheni usimuliaji wa hadithi, ngano na vipera vingine. Kwa hivyo, uwasilishwaji wa vipengele hivi kwa kutumia tarakilishi unaweza kusaidia kuamsha ari ya ujifunzaji na ufundishaji wa Fasihi Simulizi. Sababu kuu ni kwamba wanafunzi huweza kuona utendekaji na miondoko ya matendo ya Fasihi Simulizi kama nyimbo, matambiko, miviga, semi na maigizo mbalimbali kwa kutumia tarakilishi. Hali hii inaweza kusababisha kuboreka kwa kitengo cha Fasihi Simulizi katika shule za upili.

Kwa hivyo, hii ndiyo sababu kuu ya utafiti huu: kulenga matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi. Uwezeshwaji wa mradi huu utaleta uhai na utendekaji wa vitendo kama nyimbo na ngomezi darasani. Huu utakuwa uhamishwaji wa ufundishaji wa Fasihi Simulizi kutoka mazingira ya jadi ya nyumbani hadi katika darasa la sasa.

### 1.4 Malengo ya utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza nafasi ya tarakilishi katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi katika somo la Kiswahili. Malengo mahsusi yalikuwa:

i. Kutathmini ni kwa kiwango kipi tarakilishi hutumiwa kama wenzo wa kufunza Fasihi Simulizi katika shule za upili katika kaunti ya Bungoma.

ii. Kuchunguza jinsi walimu huandaa na kushirikisha tarakilishi wanapofunza Fasihi Simulizi katika shule za upili katika kaunti ya Bungoma.

iii. Kubainisha changamoto ambazo shule na walimu hukumbana nazo katika juhudi za kushirikisha tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi katika shule za upili katika kaunti ya Bungoma.

iv. Kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa shule za upili za kaunti ya Bungoma katika kufundisha Fasihi Simulizi.

### 1.5 Maswali ya utafiti

Maswali ya uatafiti yaliyoibuliwa na malengo yaliyotajwa hapo juu ni kama yafuatavyo:

i. Je, ni kwa kiwango kipi walimu hutumia tarakilishi kama wenzo wa kufunzia Fasihi Simulizi katika shule za upili za kaunti ya Bungoma?

ii. Ni vipi walimu huhusisha tarakilishi katika maandalizi na ufunzaji wa Fasihi Simulizi katika shule za upili za kaunti ya Bungoma?

iii. Ni changamoto zipi zinazozikumba shule na walimu wa Kiswahili katika kutumia tarakilishi kama wenzo wa kufunzia Fasihi Simulizi katika shule za upili katika kaunti ya Bungoma?

iv. Je, walimu wa shule za upili katika kaunti ya Bungoma hutumia mbinu zipi katika kufundisha Fasihi Simulizi katika shule za kaunti ya Bungoma?

## 1.6 Umuhimu wa utafiti huu

Inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatawasaidia walimu kujiboresha zaidi katika matumizi yao ya teknolojia za kisasa katika ufunzaji na hasa ufundishaji wa Fasihi Simulizi kwa kutumia tarakilishi. Kupitia tarakilishi mwalimu anapata ujumbe haraka zaidi; ujumbe huo ni wa haraka na anawahusisha wanafunzi wengi katika somo lake. Hali hii huwapa wanafunzi kumbukumbu nzuri ya yale waliyoyasoma. Wanafunzi huvutiwa sana na picha, michoro na vielelezo mbalimbali wavionavyo na ambavyo huwezeshwa kirahisi kwa kutumia tarakilishi.

Serikali na wadau katika elimu kama vile Wizara ya Elimu, wazazi na mashirika mbalimbali yataelewa mchango wao katika kuboresha mazingira ya ufundishaji pamoja na vyombo vya kufundishia darasani. Kilicho cha muhimu ni kuwapatia walimu mafunzo ya namna ya kutumia vyombo vya kisasa vya kidijitali kama tarakilishi ili wavitumie katika kufundisha kwao Fasihi Simulizi.

## 1.7 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya tarakilishi kama wenzo wa kufunzia. Wenzo wa tarakilishi ulilengwa kwa sababu tarakilishi ni teknolojia ngeni na ambayo imeshika mizizi katika elimu. Mabadiliko ya wakati pamoja na maendeleo ya kasi yanayoshuhudiwa ulimwenguni yanakuwa kivutio kikubwa kwa tarakilishi kuenziwa. Kifaa hiki kinapotumiwa darasani na walimu wapate tajiriba nzuri ya kukitumia, huenda wanafunzi wakanufaishwa sana shuleni.

Utafiti ulijikita katika matumizi ya tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi katika shule za upili na si vipengee vingine vya somo la Kiswahili. Vipera muhimu vilivyolengwa

ni kama nyimbo, semi, maigizo pamoja na hadithi. Kwa kutumia tarakilishi, mwalimu hupata ujumbe haraka zaidi. Ujumbe ule ni wa kisasa naye huwahusisha wanafunzi zaidi katika somo lake. Hali hii huwapa wanafunzi kumbukumbu nzuri ya yale wanayosoma na kuyashuhudia wakati wa masomo yao.

Mtafiti alijikita kwenye kipengele cha Fasihi Simulizi kwa sababu hutegemea nyenzo za kuonekana na kusikiliza na hivyo kujenga kumbukumbu bora kwa wanafunzi. Fasihi hii ni asilia kwa sababu imerithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Pia huchangia katika kuhifadhi na kuendeleza historia ya jamii kuhusu asili yake na hivyo kuwatambulisha wanafunzi. Kama ilivyo Fasihi Andishi, Fasihi Simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee unaotoa fursa njema ya kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa sababu ya nafasi yake muhimu Fasihi Simulizi inapaswa kufunzwa vyema ili wanafunzi waweze kutumia maarifa haya kutunza na kuendeleza nchi. Hata wanafunzi watafurahia kipengele hiki ikiwa kitafunzwa vyema hasa tarakilishi ikihusishwa. Utafiti huu ulifanywa katika shule teule za maeneo bunge katika kaunti ya Bungoma. Eneo hili la Bungoma liliteuliwa kwa maana lilikuwa na shule teule ambazo zingeweza kufanyiwa utafiti. Data ya kuaminika iliweza kupatikana kwa maana shule na wasailiwa walikuwepo. Hata hivyo, utafiti huu ungeweza kufanyika katika sehemu yoyote ile na data ya kuaminika ikapatikana.

Kutokana na manufaa mengi ya tarakilishi kwa ufundishaji, utafiti huu ulichunguza namna walimu hutumia tarakilishi ili kuvuna baadhi ya manufaa hayo. Baadhi ya manufaa hayo ni kama wepesi wa kufundisha vipindi, kuwafundisha wanafunzi wengi kwa pamoja na kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya kuzitumia tarakilishi baada ya masomo yao ya upili.

Utafiti huu ulijumuisha shule teule kumi na nane (18) ambazo zinapatikana katika kaunti ndogo tisa (9) zilizomo katika eneo la Bungoma. Kila eneo ndogo lina shule mbili (2) teule; ya wasichana na ya wavulana. Walimu wawili wawili walitafitiwa katika kila shule idadi yao ya jumla ikiwa walimu thelathini na sita (36). Pia, utafiti ulihusisha walimu wakuu kumi na wanane (18). Idadi hii ikiwa inawakilisha mwalimu mkuu mmoja katika kila shule. Kwa ujumla wasailiwa wote walikuwa hamsini nan ne (54).

### 1.8 Misingi ya nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ukubalifu na Matumizi ya Teknolojia (NUMT). Mwasisi wa nadharia hii ni Rogers (2003). Misingi ya nadharia hii ni kuwa ukubalifu na matumizi ya teknolojia si jambo linalofanyika wakati mmoja. Rogers anasema kwamba ukubalifu wa teknolojia mpya hutegemea mambo manne muhimu:

Kwanza, ni teknolojia yenyewe. Watumizi huchunguza ujuzi wao katika kutumia teknolojia hiyo na kama itawafaa zaidi kuliko mbinu ambazo wamezitumia awali. Kutokana na utafiti wao, wataalamu huamua kuitumia au wasiitumie.

Pili, watumizi huangalia mbinu za mawasiliano kati yao. Kwa mujibu wa Rodgers (k.h.j) watu huwasiliana kupitia vyombo tofauti vya habari na pia kwa njia ya ana kwa ana. Nadharia hii inaonyesha wazi kwamba ukubalifu wa teknolojia hutokea mara nyingi kati ya watu wa viwango tofauti vya ujuzi. Katika hali kama hiyo, huenda pakatokea msukumo wa kubadilishana mawazo, ikiwemo teknolojia iwapo itaonekana ya kufaa.

Rodgers (k.h.j) anasema kuwa jambo la tatu muhimu katika ukubalifu wa teknolojia ni muda wanaoweza kuchukua watumizi ndipo wapate umilisi na uwezo kamili wa kutumia hiyo teknolojia haraka kuliko wenzao. Hapa Rodgers (k.h.j) anamaanisha kuwa muda unachangia pakubwa ukubalifu wa teknolojia ngeni katika jamii.

Jambo la mwisho analotaja Rodgers (k.h.j) kuhusu nadharia hii ni uhusiano baina ya watumizi. Anasema kuwa watumizi hushirikiana katika nyanja tofauti za maisha yao na ikiwa teknolojia itawafaa katika mitagusano yao tofauti basi wataikubali. Anaendelea kusema kuwa watumizi wa teknolojia wanaweza kugawanywa katika makundi kadha; yaani wale wanaokubali teknolojia mara moja, wengine huikubali mwanzoni tu, ilhali wengine huikataa ile teknolojia kabisa. Maoni ya Rogers (k.h.j) ni kuwa kila teknolojia hupitia hatua kadhaa ndipo ikubaliwe na watumizi. Ingawa utafiti huu haukuchunguza hatua za ukubalifu, wazo hili lilichangia swala la kama walimu hutumia tarakilishi au la.

Nadharia hii ilifaa katika utafiti huu kwani lengo hapa ni kutathmini matumizi ya tarakilishi katika kufunza Fasihi Simulizi. Matumizi ya teknolojia hii ni mageni katika ufunzaji wa kipengele hiki. Ikiwa walimu watapitia hatua zinazopendekezwa na Rogers (k.h.j) mwishowe watakubali kutumia tarakilishi kufunzia. Ni vyema walimu kuelewa umuhimu wa tarakilishi, wapewe muda wa kufanya uamuzi binafsi kama watatumia tarakilishi au la; wapewe muda wa majaribio na kisha watafiti zaidi kuhusu teknolojia hii. Ikiwa walimu hawana ujumbe wa kutosha, ni wazi kwamba watakataa hii teknolojia mpya na kuendelea kutumia njia za zamani za kufunzia Fasihi Simulizi. Walimu wanapofanya hivi, bila shaka watakosa manufaa ya kutumia teknolojia za kisasa.

Kutokana na maoni ya Rogers (k.h.j) katika hii nadharia, hisia kuhusu matumizi ya teknolojia humwongoza mtumizi kufanya uamuzi wa kibinafsi. Walimu, ambao ni walengwa katika utafiti huu, wanastahili kuamua kutumia ama kutotumia tarakilishi kutokana na hisia zao binafsi. Walimu huchunguza ujuzi wao katika matumizi ya tarakilishi darasani ndipo wao wakubali au waendelee kutumia mitindo ya zamani kufunza.  Pia wataangalia ikiwa tarakilishi zitawarahisishia mawasiliano au kazi yao ya kufunza na hivyo kuokoa muda ambao wangetumia kutoa maelezo marefu.  Ikiwa tarakilishi ina dosari basi  wanaepuka matumizi yake polepole.

## 1.9 Muhtasari

Sura hii imejadili mambo muhimu yanayotoa msingi wa utafiti huu. Imeangazia usuli wa mada, swala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti huu pamoja na nadharia iliyouongoza utafiti huu. Sura imetoa mwelekeo ufaao kwa sura ya pili ambayo inahusu uhakiki wa maandishi yanayohusu Fasihi Simulizi na teknolojia ya tarakilishi.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilihakiki tafiti tofauti zilizofanywa kuhusu matumizi ya teknolojia na hasa tarakilishi katika ufunzaji shuleni. Uhakiki huu wa maandishi vilevile ulijikita katika tafiti zilizofanywa hapo awali kuhusu matumizi ya tarakilishi katika shule za upili. Matumizi haya ya tarakilishi hasa darasani yalikuwa na maksudi ya kuwajumuisha wanafunzi kikamilifu katika somo husika.

## 2.2 Dhana ya tarakilishi

Kila uchao ulimwengu unazidi kubadilika kwa uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Uvumbuzi ambao umeshika kasi  sasa ni matumizi ya tarakilishi katika mawasiliano. Tarakilishi ni aina ya mtambo ambao hupokea habari na kuishughulikia kulingana na kanuni za programu inayopewa. Kifaa hiki ni makini hivi kwamba huchanganua data inayopatiwa kuifanya hatua kwa hatua na kwa mantiki ya ajabu. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) tarakilishi ni chombo cha elektroniki chenye uwezo wa kupokea na kukusanya habari, kuichanganua habari hiyo na kutoa matokeo haraka sana.

Teknolojia hii ilianzishwa Ujerumani mwaka wa 1642 na Pascal kwa lengo la kufanyia hesabu. Uwezo wake wa kufanya mambo tofauti wakati mmoja ulidhihirika tena mwaka wa 1944 nchini Uingereza kifaa hiki kilipotumiwa kufanyia biashara na kuhifadhi ujumbe. Chombo hiki cha kidijitali kinaiwezesha kazi kufanyika haraka sana ajabu. Ujumbe kutoka kwa mtandao hupatikana kwa sekunde tu na kutafuta ujumbe katika sekta tofauti hutekelezwa kwa wepesi na uhakika wa juu. Sekta ya elimu haikusazwa kwani

kifaa hiki kilitumika kufanyia utafiti, kuonyesha picha za mafundisho na hata kuhifadhi ujumbe muhimu shuleni na vyuoni kama anavyodai Primo (2003).

Kutokatana na tafiti tofauti kama vile wa Young na Quinn (2003), Watson (2001) na Volman (2005), wajuzi katika sekta ya elimu huchukua muda mwingi kuandaa vifaa vya kufunzia lakini vifaa hivi havitumiwi na walengwa yaani walimu. Suala la matumizi haliangaliwi. Kwa hivyo, hakuna maelezo kamili ili walimu watumie au wasitumie vifaa vya kufunzia katika ufunzaji. Maoni haya ni muhimu kwa utafiti huu ambao ulilenga kuchunguza hasa namna walimu wanavyohusisha tarakilishi kufunza kipengele cha Fasihi Simulizi.

### 2.3 Dhana ya Fasihi Simulizi

Fasihi Simulizi ni aina ya sanaa inayotumia lugha na huwasilishwa kwa njia ya masimulizi, Wamitila (2004). Kadhalika, Fasihi hii huwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu na maisha yake katika jamii fulani. King'ei na Kisori (2003) anaifafanua Fasihi Simulizi kama sanaa maalum ya matumizi ya lugha inayotokana na usanifu, ufasaha na ufundi wa kuwasilisha ujumbe kwa njia ya masimulizi. Fasihi hii ndiyo kongwe zaidi kwani imekuweko tangu mwanzo wa binadamu. Inajumuisha hadithi za aina mbalimbali, nyimbo na ngoma za kitamaduni, tenzi fupi na sanaa za maonyesho Msokile (1993). Fasihi Simulizi ni sehemu ya utamaduni ambao huambatanishwa na mila na amali za jamii husika. Naye Wanjala (2013) ansema kuwa Fasihi Simulizi ni sanaa inayotumia lugha na matendo kuwasilisha ujumbe juu ya maisha ya binadamu.

Nchini Kenya, Fasihi Simulizi ni mojawapo ya vipengele vinavyofunzwa katika somo la Kiswahili. Kwa mujibu wa Taasisi ya Elimu Nchini Kenya (k.h.j) somo hili ni la lazima

katika shule za msingi na upili. Wanafunzi wote basi hupata nafasi ya kusoma vipengele tofauti vya Fasihi Simulizi na kufahamu tamaduni za jamii tofauti kupitia somo hili. Wamitila anasema kuwa tawi hili la fasihi hutumiwa kupashana maarifa ya utamaduni fulani, historia ya jamii, matamanio yao, mitazamo na historia yao. Fasihi Simulizi basi ndicho chombo muhimu cha jamii.

Maarifa haya ya jamii yanaweza kuwafikia wanafunzi darasani kupitia kwa somo la Kiswahili. Ni vyema basi walimu wakifunza kipengele cha Fasihi Simulizi kwa njia ambayo itawavutia wanafunzi na kuwasaidia kukumbuka tamaduni ambazo bado ni za manufaa kwao. Ikiwa tarakilishi itatumiwa kuwasilisha ujumbe wa Fasihi Simulizi darasani, vipindi vitakuwa changamfu, uhalisia utaletwa pale darasani na matokeo katika somo la Kiswahili yataboreshwa na hata tabia na mienendo ya vijana itakuwa nzuri.

**2.4 Matumizi ya vifaa vya kufunzia**

Kwa mujibu wa Brown (1986) dhana ya matumizi ya vifaa kuimarisha ufunzaji imejadiliwa tangu enzi za wasomi maarufu kama Plato. Watafiti wanakubaliana kwamba matumizi ya vifaa vya kuona na kusikiliza husaidia wanafunzi kukumbuka waliyofunzwa darasani Tucker (2007). Maoni ya Lickson (1983) ni kwamba mwalimu anapotumia vifaa tofauti kufunza, mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji darasani hubadilika. Matumizi ya kifaa hiki huondoa uchovu na ukavu na wanafunzi hupendelea mtindo huu wa kufunza. Joyce (1992) anakubaliana na maoni haya anaposema kuwa ni vyema mwalimu kuandaa mazingira tofauti kwa kila kipindi anachofunza ili kuwavutia wanafunzi. Hali hii huwasaidia sana wanafunzi ili kwamba wasichoke huku wakilichangamkia somo.

Gagne (1977) anapendekeza vifaa kutumiwa katika ufunzaji kwa vile huwatia motisha wanafunzi, naye Farrant (k.h.j) anaonelea kuwa vifaa vinavyotazamwa na wanafunzi wakati wa somo fulani huwasaidia kuelewa hali halisi ya mambo. Utafiti wa Ajeyi (1984) katika shule za Nigeria na wa Musau (1999) nchini Kenya unaonyesha kuwa walimu hutumia vifaa kama vile vitabu, vifaa halisi, chati, michoro, ramani lakini teknolojia mpya haijatafitiwa sana katika shughuli za darasani. Tafiti hizi zinaonyesha umuhimu wa kuboresha mazingira darasani kwa kutumia vifaa tofauti. Pengo hili ndilo utafiti huu unalenga kuziba.

**2.5 Matumizi ya tarakilishi darasani**

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na manufaa ya vifaa vya kufunzia. Elimu bora imehusishwa na ustadi wa walimu katika taaluma yao kulingana na maoni ya Oduro (2008). Tafiti zinazoonyesha kuwa walimu wakiboresha mazingira ya ufunzaji matokeo ya wanafunzi yataimarika. Walimu wanaweza kuboresha mazingira kwa kutumia mbinu za kisasa na hasa vifaa vya teknolojia kama tarakilishi.

Nchini Kenya, tafiti kadhaa zimefanywa zikilenga matumizi ya vifaa vya eletroniki kama vile redio, televisheni, projekta, mtandao. Hata hivyo, utafiti kuhusu namna ambavyo walimu hutumia tarakilishi ndani ya darasa kufunzia Fasihi Simulizi ni wa nadra sana Wasiche (2009). Utafiti wa sasa utajikita katika kubaini ikiwa walimu wanajua na kuzitumia tarakilishi kama kifaa cha kuchangia ufunzaji wao wa Fasihi Simulizi.

Utafiti wa Makau kuhusu matumizi ya tarakilishi darasani ulionyesha walimu kutopendelea mbinu hii. Naye Wabuyela (2003) aligundua kuwa walimu hawakupenda kutumia tarakilishi kwa sababu ya ukosefu wa vifaa hivi na ujuzi kwa upande wao. Shule

nyingi hazina vifaa vya kidijitali, zingine zikikosa nguvu za umeme huku zingine zikiwa na walimu wasio na tajiriba ya kutosheleza mahitaji ya vifaa hivi. Utafiti wa Wanjala, Khaemba na Mukwa (2011) nao unaonyesha kuwa walimu wengi hawakuwa na ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa kama tarakilishi. Tafiti hizi zililenga sababu za walimu kutotumia tarakilishi kufunzia bila kujikita katika vipengee vya masomo tofauti kama ulivyofanywa utafiti huu.

Nchini India, teknolojia ya mtandao imepewa kipaumbele. Serikali imesambaza tarakilishi katika taasisi za elimu ili zitumiwe kama vifaa vya kufunzia. Tarakilishi zinauzwa kwa bei ya chini na hata kutolewa kama msaada na mashirika yasiyo ya serikali. Kamau (2009) anasema kuwa barani Afrika shirika la NEPAD **(***New Partnership for Africa's Development*) limezindua programu ya masomo ya mtandao kwa shule za msingi na upili kwa miaka kumi (10). Jitihada hizi zimezaa matunda kwani baadhi ya shule zimepata na hata sasa hutumia tarakilishi kufunza.

Mabadiliko katika elimu hulenga kuboresha na kutoa elimu sawa kwa wananchi wote. Elimu bora huchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Matumizi ya teknolojia za kisasa na hasa tarakilishi ni jambo la lazima. Robertson (k.h.j) anasema kuwa matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji humfaidi sana mwalimu na mwanafunzi. Naye Volman (k.h.j) anasema kuwa matumizi ya tarakilishi yatasaidia kusambaza ujumbe na ujuzi muhimu katika karne ya 21. Kupitia mtandao wanafunzi wanaweza kushirikiana kwa kupashana ujumbe, na kufanya utafiti kuhusu mada tofauti Bates (2005).

Naye Wims na Lawler (2007) wakitamatisha utafiti wao walisema kuwa matumizi ya tarakilishi huboresha matokeo ya wanafunzi, mbinu za ufunzaji na kuinua kiwango

cha elimu na kwamba tarakilishi pia ni mojawapo ya vifaa vya kisasa vya kufunzia ambavyo vinastahili kutumiwa kikamilifu.

Ili kuhimiza matumizi ya tarakilishi katika shule za Kenya, serikali inashirikiana na mashirika kama vile *Nokia, Safaricom* na *Samsung* kutoa huduma za mtandao katika shule ili kuboresha mbinu za ufunzaji shuleni. Mashirika mengine kama vile *e Kitabu, ed-Tech Tablet Initiativ*e na *Tarakilishi kwa Shule za Msingi* yote yametoa tarakilishi kwa shule tofauti ili zitumiwe katika shughuli za ufunzaji. Pia shule nyingi zinaendelea kuunganishwa kwenye mtandao hasa kupitia kwa *Cyber Optic;* jambo ambalo linaamsha ari na mshawasha miongoni mwa walimu na wanafunzi kutumia tarakilishi shuleni mwao.

Hata hivyo, utafiti wa Gulbahar (2007) umeonyesha kuwa uwekezaji wowote ule si lazima kila mara usababishe matumizi ya teknolojia mpya. Kuna mambo mengine ambayo yanachangia utokeaji huu kama vile fikra na mazoea ya walimu, kuwepo kwa vifaa hivi na uwezo wa walimu kuvitumia. Dhana hii imechangia pakubwa utafiti huu. Swali hapa ni iwapo walimu wamekumbatia teknolojia mpya ya tarakilishi katika ufunzaji wao ama la.

Nchini Kenya, ili kufikia ruwaza ya 2030, ni muhimu kila mtu kuwa na ujuzi wa kutumia tarakilishi. Shule zetu hazijasazwa hapa nazo zimo mbioni kutimiza lengo hili. Lazima walimu na wanafunzi wawe na ujuzi wa kutumia teknolojia hii ili kukamilisha mitaala kwa muda, kuboresha vipindi, kufanya utafiti na kuwasiliana na wenzao katika sekta ya elimu.

Tukirejelea somo la Kiswahili ambalo ni la lazima katika shule zote nchini Kenya, walimu wanapaswa kujizatiti katika matumizi ya tarakilishi kufunza. Kipengee cha Fasihi Simulizi kinaweza kuboreshwa zaidi ikiwa walimu wanaweza kutumia tarakilishi kukifunza.

Utafiti huu ulitathmini jinsi walimu wa somo la Kiswahili hutumia tarakilishi kufunza kipengele cha Fasihi Simulizi. Kipengele hiki ni muhimu kwani kando na kuboresha alama za wanafunzi katika mtihani, huwafunza utamaduni wao. Wanafunzi hupata nafasi ya kuona, kusikia na hata kutembelea fanani walio na maarifa ya Fasihi Simulizi. Matumizi ya tarakilishi yanaleta haya yote darasani na basi kupunguza gharama ya elimu. Kulingana na Song na Kang (2012) mafundisho wanayoyaona na kuyasikia kupitia kwenye tarakilishi ni rahisi kuyakumbuka kwani yanaonyesha mfano wa hali halisi ya mambo.

## 2.6 Matumizi ya tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi

Somo la Kiswahili limegawanywa katika sehemu tofauti; insha, lugha na fasihi. Kwa mujibu wa TENK (2002) hizi sehemu huchangia alama za mwanafunzi na zinaweza kufunzwa kutumia mbinu na vifaa tofauti. Tafiti za awali zimeonyesha kuwa walimu wa Kiswahili wana vipengele vingi vya kushughulikia katika somo hili kwa hivyo hawana muda wa kutosha kutumia mbinu tofauti kufunza au kutafuta vifaa vya kufunzia. Wengi hutumia mbinu ya mhadhara na vitabu vilivyopendekezwa (k.h.j).

Utafiti wa Suter na Busienei (2013) kuhusu ufunzaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili unaonyesha kuwa walimu wengi hawakutilia mkazo kipengele cha Fasihi Simulizi. Wao waliona kama mchango wake kwa somo la Kiswahili ni mdogo sana, kwa hivyo

walisisitiza vile vipengele vingine kama lugha, insha na Fasihi Andishi. Utafiti huu pia unaonyesha kuwa hakuna vifaa vilivyotumiwa katika ufunzaji wa somo la Kiswahili isipokuwa vitabu vya kiada na vile vilivyopendekezwa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (TUMK).

Fasihi Simulizi ni kazi ambazo kimsingi hupokezwa kwa njia ya masimulizi (Wamitila 2003). Kwa mujibu wa Njogu (2006), Fasihi Simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee ambao hutoa fursa njema ya kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ndani mwake kuna masimulizi, maigizo, tathmini za mazingira na mahusiano ya kijamii.

Ikiwa Fasihi Simulizi itafundishwa kwa kuzingatia hisia zote za mwanafunzi basi itakuwa rahisi kwake kukumbuka yaliyofunzwa. Hata uhalisia unaweza kufikika ikiwa teknolojia kama tarakilishi inaweza kutumiwa darasani.

Kulingana na utafiti wa Mrikaria (2007) uliofanywa nchini Tanzania, teknolojia za kisasa zinaweza kutumiwa kuhifadhi Fasihi Simulizi. Kulingana na utafiti huu, Fasihi Simulizi iliyohifadhiwa kwa kutumia teknolojia ni ya hali ya juu na inaweza kuwafikia watu wengi katika maeneo tofauti kwa wakati mfupi ajabu. Kando na utafiti huu kuorodhesha umuhimu wa kuhifadhi Fasihi Simulizi, haukuzungumzia kama vifaa vya teknolojia vinaweza kutumiwa kama mbinu ya ufunzaji. Utafiti huu umeandaliwa ili kuziba pengo la matumizi ya teknolojia na hasa tarakilishi kufunza Fasihi Simulizi darasani. Ni wazi kwamba mambo yaliyohifadhiwa yanaweza kuwasilishwa kwa wanafunzi, na mbinu hii inaweza kuwavutia wanafunzi sana.

Wetende (2015) alitafiti matumizi ya nyenzo tofauti katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi. Alipata kwamba shule nyingi hazina nyenzo anuai, walimu walitumia vitabu tu navyo

vilikuwa vichache. Utafiti huu haukuchunguza vifaa mbadala na hasa teknolojia za kisasa kama tarakilishi. Kwa upande mwingine utafiti wa Wanjuki (2000) kuhusu ufunzaji wa fasihi katika shule za jiji la Nairobi aligundua kwamba baadhi ya shule zilikuwa na nyenzo za kisasa za kufunzia kama redio, televisheni na video. Hata hivyo, walimu hawakutumia nyenzo hii kwa shughuli za ufunzaji.

Rotumoi (2006) pia alitafiti kuwepo na matumizi ya nyenzo za kufunzia Fasihi Andishi. Alipata kwamba nyenzo tofauti zilikuwepo katika shule lakini walimu wengi wa lugha hawakupenda kuzitumia. Basi ni muhimu kuufanya utafiti huu ili uweze kuangazia kipengele cha Fasihi Simulizi.

Agufana (2000) pia katika utafiti wake alipata kuwa shule zina nyenzo tofauti za kufunzia Fasihi Simulizi lakini walimu hawakuzitumia mara nyingi. Ni walimu wachache sana ambao walizitumia nyenzo hizo katika kufunzia vipengele mbalimbali shuleni.

Maranga (1993) anatilia mkazo kwamba wanafunzi wanaweza tu kuelewa ikiwa mwalimu atahusisha nyenzo tofauti katika ufunzaji wake. Tahir (2002) katika utafiti wake kwa jamii za kuhamahama nchini Nigeria alipata kwamba hata vitabu vilikuwa vichache na walimu walitumia tu chaki na ubao. Nyenzo muhimu za ufunzaji na hasa tarakilishi ni haba katika shule za kuhamahama.

Too (1996) alitafiti kuwepo kwa nyenzo za kufunzia hesabu katika wilaya ya Nandi na akapata kwamba zilikuwa chache; jambo ambalo huenda lilichangia matokeo duni katika somo hilo. Awali, Mukwa (1979) katika utafiti wake aligundua kwamba nyenzo za kufunzia ni chache katika shule nyingi ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi ambao waliongezeka kila mwaka. Kafu (2000) alipata katika utafiti wake kuwa nyenzo ni

chache na hutumiwa zaidi na walimu katika shule za umma tofauti na wale wanaofunza katika shule za kibinafsi.

Chesaina (2007) anasema kuwa elimu ya awali anayopata mtoto humfunza tabia zinazokubalika na utamaduni wa jamii yake. Fasihi Simulizi inaweza kutumiwa kumuadilisha mtoto kuanzia anapokuwa mdogo hadi anapokuwa mtu mkubwa. Anapendekeza kwamba somo la Fasihi Simulizi lifunzwe vizuri kwa kutumia nyenzo tofauti ambazo zinaweza kuwavutia watoto.

Akivaga na Odaga (1985) wanasema kuwa shule nyingi zimewanyima nafasi wanafunzi kufurahia somo la Fasihi Simulizi kwa uhaba wa nyenzo na hata nafasi za kuzuru sehemu zenye maonyesho ya utamaduni wetu. Haya yamechangia kudorora kwa viwango vya elimu. Walimu wengi hutumia tu mbinu ya mhadhara kufundisha ili kukamilisha silabasi katika kipindi walichotengewa ambacho huchukua dakika arobaini. Mbiti na Ayot (1984) wanasema kuwa kufundisha hivi ni sawa na kuangamiza Fasihi Simulizi. Nandwa na Bukenya (1990) wanapendekeza kuwa lazima walimu waandae mazingira ya kuwavutia wasomi na hata kuwapa nafasi kutoa maoni na tajriba zao kuhusu Fasihi Simulizi.

Tafiti ambazo zimerejelewa zimefafanua nyenzo kwa jumla na umuhimu wake katika ufunzaji. Pia zimeonyesha kuwa uhaba wa nyenzo na walimu kuzipuuza umesababisha kutozishirikisha nyenzo katika ufunzaji. Tafiti hizi hazikurejelea teknolojia za kisasa, ikiwemo tarakilishi na nafasi yake katika muktadha wa ufunzaji.

Kwa hivyo lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza kama manufaa ya Fasihi Simulizi yanaweza kuwafikia wanafunzi kupitia kwa matumizi ya tarakilishi darasani. Tafiti za awali zimeonyesha tu kwamba Fasihi Simulizi ni muhimu na inafunzwa darasani bila

kudokeza kama teknolojia ya kisasa kama tarakilishi pia inaweza kutumiwa kufunzia kipengee hiki.

### 2.7 Muhtasari

Katika sura hii, Mtafiti amefafanua dhana ya tarakilishi na kuonyesha matumizi ya teknolojia katika taaluma ya elimu. Pia, amerejelea tafiti ambazo zimefanywa kuhusu matumizi ya tarakilishi katika sekta mbalimbali hasa elimu. Mtafiti ameonyesha pengo la utafiti kuhusu matumizi ya tarakilishi katika kufunzia Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Sura ifuatayo inaelezea mchakato na mbinu zilizotumika katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inajumlisha mbinu zilizozingatiwa katika utafiti huu. Hasa imefafanua muundo na eneo la utafiti, wasailiwa, mbinu za usampulishaji, mbinu za kukusanya data, uhalali na ubora wa vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data na maadili ya kiutafiti.

## 3.2 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ulizingatia muundo wa kithamano mkabala wa usoroveya. Utafiti wa kithamano huegemea maelezo na kutolea mifano katika majedwali. Muundo wa kithamano humwongoza Mtafiti kukusanya habari kwa kuhoji wasailiwa ama kukipatia kikundi fulani cha wasailiwa hojaji ili wazijaze Orodho (2003). Utafiti uliegemea muundo wa kithamano huku ukiegemea sana mkabala wa usoroveya. Muundo huu wa utafiti hukusanya habari kwa kuuliza maswali na kujaza hojaji. Maoni ya wasailiwa hutumiwa kutoa uamuzi kuhusu jambo linalotafitiwa. Usoroveya unaweza kutoa data ya kimaelezo au ya kihesabu na ujumbe huo ukatumiwa kueleza hali halisi ilivyo kama anavyosema Mtafiti Nsubuga (2000). Oso na Onen (2005) nao wanasema kwamba muundo huu wa utafiti ni bora zaidi kwani unasaidia pakubwa kukusanya data inayoonyesha ukweli na uhalisia wa suala la utafiti. Halikadhalika, muundo huu hufwata utaratibu maalumu na hivyo kutoa ujumbe wa kuaminika. Muundo huu ulimsaidia Mtafiti kutathmini matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi. Mtafiti alizingatia muundo huu kwa sababu ni rahisi kufanya utafiti kwa utaratibu maalumu kulingana na malengo ya utafiti. Pia, huu muundo ungeonyesha hali halisi ya ufunzaji katika shule.

### 3.3 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika kaunti ya Bungoma ambayo ni mojawapo ya kaunti arobaini na saba (47) nchini Kenya. Kaunti hii imo katika eneo la Magharibi katika mpaka wa nchi ya Kenya na nchi ya Uganda. Upande wa kusini inapakana na kaunti ya Busia; Mashariki ni Kakamega na Kaskazini ni kaunti ya Trans Nzoia. Kuna kaunti ndogo tisa (9) na maeneo-bunge tisa (9). Wakaazi wa eneo la Bungoma ni wa mchanganyiko. Kuna jamii ya Wabukusu wanaongea lugha ya Kibukusu, jamii ya Wateso wanasema lugha ya Iteso, jamii ya Wasabaoti ambao hunena Kisabaoti pamoja na Watachoni wanaongea Kitachoni. Kwa sababu ya ukarimu wa jamii hizi, jamii nyingine za Kenya zimefika Bungoma na kuchangamana na wenyeji. Kwa hivyo basi hii ni sehemu iliyosheheni mchanganyiko wa lugha huku lugha ya Kiswahili ikishika mizizi. Wenyeji hujishughulisha sana na kilimo cha mazao na mifugo. Wengi hupanda miwa na mahindi (Bungoma 2007, Kenya Bureau of Statistics).

Kupitia mpango wa usambazaji umeme mashinani, sehemu nyingi zinapata huduma hii. Hata shule nyingi zimefaidika kutokana na mpango huu. Kaunti hii ina takriban watu 1,375,063. Asilimia hamsini na tatu (53%) ya watu hawa wanaishi katika hali ya umaskini. Kwa mujibu wa Ofisi ya Mkuu wa Elimu katika kaunti ya Bungoma (2014) kuna shule mia tisa (900) za msingi, mia mbili sabini (270) za upili na vyuo anuai arubaini na nane (48). Idadi ya wanafunzi katika shule za msingi ni takribani elfu mia moja ishirini na tatu (123,000) na elfu sitini na nane (68,000) katika shule za upili. Idadi ya walimu katika shule za upili ni elfu moja mia tatu (1,300).

Mtafiti alichagua kufanya utafiti katika kaunti hii kwa sababu Bungoma ni kaunti mojawapo kubwa katika Kenya. Kwa hivyo basi ilifaa sana kwamba wasailiwa lengwa wanaweza kutoa picha halisi ya matumizi ya tarakilishi katika taifa la Kenya kwa ujumla.

Isitoshe, Kiswahili kinafundishwa kama somo katika shule za upili. Vilevile mtaala wa somo la Kiswahili kama lilivyoandaliwa na TUMK ni ule ule. Halikadhalika, shule teule zina vifaa vya tarakilishi ambavyo Mtafiti alitarajiwa kuvifanyia utafiti wake. Pia, teknolojia za kisasa zimeshika kasi katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu. Mtafiti alinuia kutathmini ni kwa kiwango kipi walimu hushirikisha teknolojia mpya katika ufunzaji ikiwemo tarakilishi. Pia, Kiswahili ni somo la lazima kwa wanafunzi wote kwa hivyo lazima idadi yao ni kubwa. Wasailiwa walengwa katika mazingira haya ya shule teule walitarajiwa kuwa na ujuzi wa kutumia tarakilishi. Mtafiti alitaka kufahamu kama walimu hushirikisha tarakilishi kazini mwao kwani ni wenzo mzuri wa kufunzia hasa kwa madarasa ya wanafunzi wengi. Kulingana na Singleton (1993), ni vyema kama Mtafiti achague eneo ambalo litamsaidia kupata data inayofaa utafiti wake, anaweza kulifikia eneo hilo kwa urahisi na pia anaweza kuwa na mlahaka mzuri na wasailiwa. Maoni haya yalichangia Mtafiti kufanya utafiti wake katika kaunti ya Bungoma.

### 3.4 Wasailiwa lengwa

Utafiti huu ulilenga shule zote mia mbili sabini (270) za upili katika kaunti ya Bungoma zilizo na wanafunzi elfu sitini na nane (68,000). Idadi ya walimu nayo ikiwa takribani elfu moja mia tatu (1,300). Shule hizi zimegawanywa katika makundi kama vile shule za umma na za kibinafsi, za mchana na malazi. Pia kuna za wasichana pekee, wavulana peke na hata za mseto. Kuna shule mbili za kitaifa, zile za kaunti na maeneo ya nje, za kaunti na kaunti ndogo. Kaunti hii ina shule teule kumi na nane (18)

zilizopandishwa vyeo miaka michache iliyopita kulingana na mapendekezo ya Wizara ya Elimu kuhakikisha kuwa serikali inatoa kiwango cha juu cha elimu kwa wanafunzi wengi. Serikali iliamua kupandisha vyeo shule mbili katika kila kaunti ziwe za kitaifa. Pia ikapandisha vyeo shule mbili katika kila eneo bunge ziwe shule teule. Hizi ndizo shule alizozilenga Mtafiti katika uchunguzi wake.

Utafiti huu ulishirikisha shule kumi na nane (18) teule za kaunti ya Bungoma. Sababu ni kuwa shule hizi zilipata ufadhili kutoka kwa serikali ili kuboresha miundo msingi, vifaa vya kufunzia na hata kuboresha mazingira ya masomo. Hii inatokana na juhudi za serikali kuboresha kiwango cha elimu katika sehemu nyingi iwezekanavyo. Ni shule kumi na nane (18) zilizoshirikishwa katika utafiti huu kwani kila kaunti ndogo ina shule mbili zilizoteuliwa. Mtafiti alipata kwamba kutokana na ufadhili wa serikali kila mojawapo ya shule hizi ina tarakilishi ambazo hutumiwa katika shughuli za kufunza.

Wasailiwa walikuwa walimu wa somo la Kiswahili na walimu wakuu wa shule za upili teule. Idadi ya wasailiwa ilikuwa hamsini na nne (54), ikiwa na maana kwamba walimu wakuu walikuwa kumi na wanane (18) na walimu wa Kiswahili thelathini na sita (36).

### 3.5 Sampuli na usampulishaji

Kwa vile idadi ya wasailiwa lengwa ilikuwa kubwa Mtafiti alichagua sampuli ndogo kuiwakilisha. Kutokana na sampuli hii, matokeo yanaweza kujumlishwa kwa wasailiwa wote. Mbinu za kuchagua sampuli zilikuwa zifwatazo.

### 3.5.1 Sampuli kusudio

Mbinu hii hutumiwa kuchagua wasailiwa walio na ujumbe muhimu unaoafiki malengo ya utafiti. Hii hupunguza gharama na muda. Katika utafiti huu mbinu hii ilitumiwa kuchagua kaunti ya Bungoma, shule za upili teule za kaunti ndogo na walimu walioshirikishwa katika utafiti. Sababu za kuchagua kaunti hii ni kuwa Mtafiti angewafikia wasailiwa kwa urahisi ili kurahisisha shughuli ya kukusanya data. Pia shule za upili katika kaunti hii huzingatia mtaala wa taasisi ya elimu nchini na Kiswahili ni somo la lazima kwa kila mwanafunzi. Utafiti huu ulifanywa kimaksudi katika shule teule za kaunti ndogo kwa vile zimepewa ufadhili wa ziada na serikali kuboresha miundo msingi na mazingira ya kusoma. Kwa hivyo Mtafiti alitarajia kwamba shule hizi zina vifaa vya kisasa vikiwemo tarakilishi za kutumiwa kufunzia. Walimu wa Kiswahili walilengwa kimaksudi kwa sababu ni wao wanaofunza Fasihi Simulizi na wangetoa ujumbe muhimu kwa utafiti huu. Walimu wakuu walichaguliwa kimaksudi kwa sababu ni wao hutoa mwelekezo wa matumizi ya fedha shuleni na hivyo kuchangia kuboresha mazingira ya kufundishia.

### 3.5.2 Usampulishaji nasibu tabakishi

Utafiti huu pia ulizingatia sampuli nasibu tabakishi. Mbinu hii hugawanya watafiti katika makundi yenye mfanano fulani. Kwa kutumia mbinu hii Mtafiti aligawanya shule katika makundi k.v zile za umma na kibinafsi, za kaunti ndogo, za wasichana na za wavulana. Kisha Mtafiti alitumia lile kundi la shule teule za kaunti ndogo. Mbinu hii inafaa zaidi kwani ina uwezo wa kuonyesha tofauti zinazoweza kutokea katika kundi na kusimamia watafiti lengwa. Pia, hutumia idadi ndogo ya wasailiwa kutoka kwa kundi lote na hivyo ufadhili na muda mchache kutumiwa katika utafiti. Ina uwezo wa kuwakilisha wasailiwa wote vyema zaidi Gay (2000).

### 3.5.3 Usampulishaji nasibu

Mbinu hii huwezesha sampuli kuchaguliwa bila ubaguzi. Kila Mtafitiwa lengwa ana nafasi sawa ya kushirikishwa katika sampuli. Kupitia mbinu hii wasailiwa wanachaguliwa kutoka kwa orodha au kundi la nambari au majina. Mtafiti alitumia mbinu hii kuwateua walimu walioshiriki katika utafiti huu. Kwa vile kuna walimu kadhaa wanaofunza Kiswahili katika shule zilizoteuliwa kwa utafiti huu, Mtafiti aliandaa vijikaratasi vilivyoandikwa "ndio" au "la" kwa kundi la walimu wa kiume na vingine kwa kundi la walimu wa kike. Kisha walimu waliviokota na wale waliookota vilivyoandikwa "ndio" basi walishiriki katika utafiti. Kupitia mbinu hii Mtafiti alipata walimu thelathini na sita (36) ambao walishiriki katika utafiti huu. Ni walimu wawili (2) walioshiriki kutoka kwa kila shule iliyoteuliwa.

### 3.6 Mbinu za kukusanya data

Mbinu za kukusanya data ni zile ambazo Mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti. Utafiti huu ulitumia mbinu za aina tatu. Mtafiti aliamua kutumia mbinu hizo kwa ajili ya kupata uthabiti wa matokeo ya utafiti. Mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni hojaji na mahojiano na utazamaji.

### 3.6.1 Hojaji

Oso na Onen (k.h.j) wanadai kuwa hojaji ni maswali ambayo Mtafiti huwauliza wasailiwa (tazama Kiambatisho 1 na 2). Wasailiwa wanapata nafasi ya kusoma na kujibu maswali wanavyofikiria. Watafiti wengi wanaweza kufikiwa kwa kutumia hojaji. Hojaji inaweza kushughulikia maswali tofauti na ni rahisi kuchanganuliwa. Inaweza kuwafikia watu wengi zaidi na pia watafiti hujibu maswali yanayofanana (Kothari 2003). Huchukua muda mchache tu kujazwa. Utafiti huu ulitumia hojaji

iliyoandaliwa na Mtafiti mwenyewe kulingana na malengo ya utafiti. Mtafiti alitembelea shule zilizoteuliwa kwa utafiti huu na baada ya kupata idhini kutoka kwa walimu wakuu na walimu wa Kiswahili aliwapa hojaji zao tofauti wazijaze. Baada ya kujaza Mtafiti alizikusanya na kuziweka kwa shughuli ya uchanganuzi baadaye. Data iliyotokana na hojaji (tazama Kiambatisho cha 1 na cha 5) ilimsaidia Mtafiti kujua namna walimu hujiandaa na kutumia tarakilishi kufunza fasihi simulizi.

### 3.6.2 Mahojiano

Mahojiano ni maswali anayoulizwa Mtafitiwana kuyajibu kwa mazungumzo (tazama Kiambatisho 4). Mbinu hii humwezesha Mtafiti kupata maoni kamili na hata hisia za Mtafitiwa. Mtafiti ana uhuru wa kufafanua maswali na kumwelekeza Mtafitiwa ili apate ujumbe unaolenga madhumuni ya utafiti. Mahojiano yanaweza kuwa ya ana kwa ana, kwenye simu au wavuti. Mtafiti anaweza kupata ujumbe wa ndani na ambao hauonekani moja kwa moja au Mtafitiwa hatauandika. Katika utafiti huu mbinu hii ilitumiwa kupata ujumbe kuhusu kuwepo kwa tarakilishi shuleni, namna walimu wanavyoandaa vipindi na matumizi ya teknolojia hii kufunza Fasihi Simulizi. Pia, walihojiwa kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wanapojaribu kutumia teknolojia hii kufundisha. Mtafiti aliandaa maswali ya mahojiano na kuwaomba wale walimu waliojaza hojaji kushiriki katika mahojiano haya. Data kutokana na mahojiano ilimsaidia Mtafiti kueleza matayarisho, matumizi na changamoto za kutumia tarakilishi kufunza Fasihi Simulizi.

## 3.7 Uhalali na ubora wa vifaa vya utafiti

Sehemu hii inashughulikia vipengele vya kuhalalisha na kuthibitisha data ili iweze kuaminika na kukubalika.

### 3.7.1 Utafiti wa awali

Mugenda na Mugenda (2003) wanadai kuwa uthabiti ni kiwango ambacho kifaa cha utafiti kinaweza kutoa matokeo yaliyo sawa baada ya majaribio kadhaa. Utafiti majaribio hufanywa kwa sampuli ndogo iliyochaguliwa. Hii inafanana na sampuli kuu itakayotumiwa katika utafiti wenyewe. Uthabiti husaidia kuonyesha namna maswali yataeleweka na wasailiwa lengwa, mpangilio wa maswali na jinsi yanavyolenga madhumuni ya utafiti. Utafiti majaribio ulifanywa mwanzoni mwa Agosti 2016. Lengo lilikuwa ni kukusanya data mapema ili kubaini ufaafu wa vifaa vya utafiti kabla ya utafiti mkuu kufanywa. Majaribio haya yalifanywa katika shule mbili za kitaifa katika kaunti ya Bungoma, zikiwa Shule ya Upili ya Wavulana ya Kamusinga na Shule ya wasichana ya Lugulu. Shule hizi mbili hazikuhusishwa katika utafiti wenyewe kwani hazimo katika kitengo cha shule teule.

Mtafiti aliamua kufanya utafiti katika shule hizi kwa sababu ni za kitaifa na zina ufadhili mkubwa kutoka kwa serikali. Miundo msingi yake na vifaa vya kufunzia ni bora kwa hivyo Mtafiti angelinganisha na zile za kaunti ndogo ambazo zimeteuliwa majuzi. Pia, walimu katika shule hizi hufunza Kiswahili kama walimu wa shule za kaunti ndogo kwa hivyo ingekuwa rahisi yeye kulinganisha maandalizi ya walimu hawa wote. Matokeo yalimsaidia Mtafiti kuboresha vifaa vya utafiti kabla ya utafiti mkuu. Pia, Mtafiti alipata mwanga kuhusu maandalizi ya usafiri wakati wa utafiti mkuu.

### 3.7.2 Uhalali wa matokeo

Maana ya uhalali ni kiwango cha namna kifaa kinaweza kupima kile kilichokusudiwa kukipima. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (k.h.j), uhalali ni kiwango

kinachopatwa kutokana na uchanganuzi wa data na namna kinavyowakilisha mada inayotafitiwa. Mtafiti aliwashirikisha watafiti wenye ujuzi na tajriba katika Idara ya Kiswahili, Chuoni Kibabii ili kufanya marekebisho yanayostahili na kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vingesaidia kukusanya data iliyokusudiwa.

### 3.7.3 Utegemezi wa vifaa

Utegemezi ni kiwango ambacho kifaa cha utafiti kinaweza kutoa matokeo yaliyo sawa baada ya majaribio kadhaa Orodho (k.h.j). Matokeo yake yalisaidia sana katika kufanyia marekebisho hali yoyote tata kabla ya utafiti kufanywa. Matokeo ya utafiti majaribio yalisaidia kuhakikisha kwamba vifaa vya utafiti vingetoa matokeo ya kutegemewa.

## 3.8 Uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo

Data katika utafiti huu ilichanganuliwa kwa mkabala wa kithamano. Kwa mujibu wa Enon (1998), mkabala wa kithamano ni mbinu ya kuchanganua data ambayo Mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Naye Kress (2008) anafafanua mkabala wa kithamano kuwa unaelezea vipi na kwa nini matukio yametokea. Mkabala huu ulitumika kwa vile kulikuwa na data iliyotokana na majibu ya kimaelezo yaliyogusa maoni ya wahojiwa. Kwa hivyo, data hiyo ilihitaji kutolewa maelezo. Data iliyopatikana iliwasilishwa kwa kutumia maelezo na majedwali.

Data iliyokusanywa ilipangwa kwa utaratibu ili kuwezesha uchanganuzi kufanywa. Mtafiti alitumia njia ya kitarakimu kuchanganua ile data kisha akaiwasilisha kwa kutumia idadi, asilimia, majedwali pamoja na maelezo ili kuwezesha ile data kueleweka. Uchanganuzi huu ulimsaidia Mtafiti kujadili matokeo, kufafanua na hata kutoa mapendekezo kuhusu yale matokeo.

### 3.9 Changamoto za utafiti

Ingawa utafiti huu ulifaulu katika kutimiza malengo yake, Mtafiti alikumbana na changamoto kadha ambazo kwa kiasi ziliutatiza utafiti. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

Kwanza, upana wa kaunti. Kaunti ya Bungoma ni kubwa na kwamba Mtafiti alikuwa akizichunguza shule teule katika maeneo bunge yote tisa katika kaunti nzima ilimaanisha kusafiri sana. Baadhi ya shule kama vile Lukhuna zinapatikana ndani sana kusikokuwa na huduma nzuri ya usafiri. Kwa hivyo ilimbidi Mtafiti kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kukodisha gari la kumwezesha kuzifikia shule hizo zote kumi na nane kwa muda uliofaa.

Pili, baadhi ya wasailiwa hasa walimu wakuu walikuwa wagumu kupatikana huku wakidai kuwa hawakuwa na muda wa kuwashughulikia wageni. Ukweli ni kwamba walimu hawa walionekana kukabiliana na kazi nyingi kila mara Mtafiti alipofika kuwaona. Wengine walimtengea muda mchache sana ili washughulikie kazi zingine za utawala. Uharaka huu ulimaanisha kutopata majibu ya kina kuhusu mada fulani ambazo zilihitaji maelezo marefu. Kwa hivyo Mtafiti akafanikiwa kutumia mbinu ya hojaji badala ya mahojiano na akaweza kukusanya data nzuri.

Tatu, ukosefu wa makala ya kutosha ya kurejelea kama vile vitabu vya kudurusu pamoja na tasnifu zilizofanywa hapo awali. Hali hii ilimlazimisha Mtafiti kwenda mbali ili kutafuta makala ambayo yangemsaidia. Sehemu alizozizuru zilikuwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Masinde Muliro na Chuo Kikuu cha Moi. Hii ilimgharimu sana pesa na akatumia muda mrefu.

Hata hivyo, Mtafiti alifanya juhudi akisaidiwa na walimu wakuu aliowatembelea ambao waliufanya utafiti wake kufikia hatua nzuri. Mtafiti alikuwa mvumilivu katika kuwangoja wasailiwa kuzimaliza kazi zao ili awahoji ama awapatie hojaji kuzijaza. Kwa kuzingatia utaratibu huu, Mtafiti aliweza kukamilisha utafiti wake kwa wakati uliokuwa mwafaka licha ya kukumbwa na matatizo ya hapa na pale.

### 3.10 Maadili ya kitafiti

Kuhusu maadili ya utafiti, Rubin na Rubin (1995) wanasema ni mbinu zinazotumiwa kukusanya data pamoja na kuwasilisha matokeo ya utafiti ambayo ni ya kuaminika bila ya kuwadhuru wasailiwa. Mtafiti alitafuta kibali kutoka kwa taasisi husika na wasailiwa kabla ya kufanya utafiti. Alipewa kibali kutoka kwa Shule ya Shahada za Juu (SSJ) katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Pia alipata kibali kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Sayansi Uvumbuzi na Teknolojia (BKSUT). Baada ya kupatiwa kibali cha kufanya utafiti alikiwasilisha kwa msimamizi wa Elimu katika kaunti ya Bungoma ndipo akaanza shughuli ya utafiti. Alipofika katika shule zilizoteuliwa aliomba ruhusa kutoka kwa mwalimu mkuu na walimu kabla ya kuwapa hojaji, kuwahoji na kutazama maandalizi ya vipindi vyao. Mtafiti alifwata ratiba ya kila shule husika.Walimu wakuu na wa Kiswahili walishirikiana naye sana katika utafiti huu.

### 3.11 Muhtasari

Sura hii imeeleza hatua kwa hatua jinsi ambavyo utafiti huu ulifanywa. Mtafiti amezingatia eneo la utafiti, sampuli na mbinu za usampulishaji, mbinu za kukusanya data, uhalali na ubora wa vifaa vya utafiti. Pia, amefafanua jinsi ambavyo data ilikusanywa na maadili ya kitafiti yalivyotekelezwa. Inaonyesha namna ambavyo data ilichanganuliwa na ufafanuzi wa data hiyo. Sura ambayo inafuata itashughulikia matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Shabaha kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi katika shule teule za upili katika kaunti ya Bungoma. Sura hii inawasilisha na kufafanua data iliyokusanywa kwa kuzingatia malengo maalum ya utafiti kama ambavyo yameorodheshwa hapa chini.

i. Kutathmini ni kwa kiwango kipi tarakilishi hutumiwa kufunza Fasihi Simulizi katika shule za upili kaunti ya Bungoma.

ii. Kuchunguza jinsi walimu huandaa vipindi na kushirikisha tarakilishi wanapofunza Fasihi Simulizi katika shule za upili kaunti ya Bungoma.

iii. Kubainisha changamoto ambazo shule na walimu hukumbana nazo katika juhudi za kushirikisha tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi katika shule za upili kaunti ya Bungoma.

iv. Kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa shule za upili za kaunti ya Bungoma katika kufundishia Fasihi Simulizi kaunti ya Bungoma.

## 4.2 Viwango vya matumizi ya tarakilishi katika kufundishia Fasihi Simulizi

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini matumizi ya tarakilishi katika kufunza Fasihi Simulizi. Ili kuafikia lengo hili Mtafiti aliwateua kinasibu walimu wa Kiswahili wawili katika kila shule iliyosampulishwa kama kulikuwa na tarakilishi katika shule zao (tazama Kiambatisho 4, swali la 5). Walimu wote walikiri kuwa shule zao

zilikuwa na tarakilishi. Hata walimu wakuu walikubaliana na wazo hili. Mtafiti alithibitisha kuwa kweli kulikuwa na tarakilishi katika shule teule kwani Mtafiti aliziona hasa ofisini. Walimu wakuu kumi na tano (15) kati ya kumi na nane (18) walikuwa wamefanya juhudi kuzitafutia shule zao mitambo hiyo ya tarakilishi. Watatu (3) kati yao walisema kuwa wamo katika maandalizi ya kuzipata tarakilishi hizo haraka iwezekanavyo. Katika hojaji (tazama Kiambatisho 6), walimu wakuu walidai kuwa walinunua tarakilishi kutokana na ufadhili wa serikali, wadhamini pamoja na karo ya wanafunzi. Kwa sababu ya wao kuelewa umuhimu wa tarakilishi ndipo walizinunua katika shule zao (tazama Jedwali 4.1 ).

**Jedwali 4.1: Tarakilishi zitumikazo na zilizoharibika shuleni**

| | Tarakilishi zitumikazo | % | Tarakilishi zilizoharibika | % |
|---|---|---|---|---|
| Shule za wasichana | 90 | 16 | 120 | 22 |
| Shule za wavulana | 135 | 24 | 210 | 38 |
| **Jumla** | **225** | | **330** | |

Jedwali 4.1 linaonyesha idadi ya tarakilishi zinazotumika na zilizoharibika shuleni.

Pia, Mtafiti aliwauliza wasailiwa (walimu wakuu) kuhusu kazi ambazo hutekelezwa na tarakilishi katika shule zao naye aliyapata matokeo yafwatayo:

Shughuli za ofisi kama vile kuandika barua rasmi, kuandika nakala za mikutano ya walimu, wazazi na halmashauri ya shule pamoja na mikutano ya Wizara ya Elimu.

Kuchapisha mitihani ya shuleni kama vile mijarabu, mitihani ya kushitukiza na mitihani ya mwisho wa muhula ama mwisho wa mwaka. Pia, walimu huzitumia katika maandalizi ya maazimio ya kazi, maandalio ya masomo pamoja na nukuu za walimu.

Kufunza somo la tarakilishi ambalo limo katika mtaala wa masomo ya upili. Somo hili hufunzwa katika baadhi ya shule za upili kama somo lingine lile.

Shughuli za utafiti hasa kwa kutumia mtandao wa *Google*. Habari nyingi kuyahusu masomo takribani yote yanayofundishwa shuleni hivi sasa inapatikana katika mtandao wa *Google* na mitandao mingine kama *Yahoo!* Kwa hivyo, tarakilishi husaidia sana kuzitafuta habari hizi ambazo husaidia kukuza masomo shuleni.

Kuonyesha video za Fasihi hasa vitabu vya Fasihi Andishi ambavyo hutahiniwa kila mwaka. Vitabu vya sasa vinavyotahiniwa ni *Tumbo Lisiloshiba, Kigogo* na *Kidagaa Kimemwozea*. Maelezo ama uigizaji wa vitabu hivi kwa msaada wa tarakilishi husaidia sana kupasha habari muhimu kwa wanafunzi.

Kufanyia mazoezi ya kupata ujuzi wa kutumia tarakilishi. Hali hii huwahusu sana walimu walio na tamanio la kuboresha uwezo wa matumizi yao ya mitambo ya tarakilishi.

Tamasha mbalimbali shuleni zinazohusisha burudani, kuonyeshwa kwa video na michezo kunawezeshwa na matumizi ya tarakilishi. Vipengele hivi vinaweza kupakuliwa moja kwa moja kutoka katika tovuti ama kununuliwa kama kanda huku vikionyeshwa kwa wanafunzi moja kwa moja.

Hata hivyo, matokeo haya ya kuwepo tarakilishi shuleni hayakuonyesha kama walimu hutumia tarakilishi hizo darasani ama la. Tarakilishi huchukuliwa kama kifaa cha

kufanyia shughuli zingine na sio shughuli ya kufunza darasani. Huu ni ushahidi kuwa walimu wa Kiswahili wamekwama katika mbinu za zamani za kufunzia Fasihi Simulizi kama vile mihadhara, maelezo na maswali na majibu. Mbinu hizi haziwezi kutosheleza mahitaji ya sasa ya kidijitali. Hivi sasa wanafunzi wengi wamekuwa wazoefu wa vyombo vya kielektroniki huku wakiwa na hamu kubwa ya kutalii mawanda mapya ya maarifa. Wanafunzi hawa wamelelewa katika mazingira ya kiteknolojia ya sasa hasa katika upande wa matumizi ya tovuti. Kwa hivyo, wanafunzi wa aina hii huhitaji kuenenda na wakati. Jambo hili basi linalazimu mbinu zibadilishwe bali si kuegemea katika uzamani pekee. Katika kutumia tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi, video pamoja na vinuruweo vinatumika na kurahisisha utazamaji wa vitendo kutoka kwa wasanii ama magwiji wa sanaa mbalimbali za Fasihi Simulizi kama vile nyimbo na usimuliaji wa hadithi. Pia, kunaweza kuwepo manufaa mengine mengi tu kama vile kuokoa muda na kuboresha uwasilishwaji wa masomo na vipindi vya Fasihi Simulizi. Mtazamo huu unakubaliana na utafiti wa Tucker (2007) aliyesema kwamba matumizi ya vifaa vya kuona na kusikiliza husaidia wanafunzi kuelewa waliyofunzwa darasani na kuyahifadhi vyema katika kumbukumbu zao.

Baada ya kubaini kuwa tarakilishi hazikutumiwa kufundishia somo la Fasihi Simulizi, Mtafiti waliwauliza walimu kutaja nyenzo ama vifaa walivyotumia. Walimu wakataja nyenzo kama uigizaji, ziara za kitaaluma n.k. (tazama Kiambatisho 10)

Mtafiti aliwauliza walimu wakuu kama walimu wao walikuwa na ujuzi wa kutumia tarakilishi na wote wakakubali (tazama Kiambatisho cha 6 swali la 6). Walipoulizwa kama walimu hawa hutumia tarakilishi darasani, matokeo yakawa jinsi yameonyeshwa katika Jedwali 4.2.

**Jedwali 4.2: Matumizi ya tarakilishi kufunzia**

| **Walimu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Watumiao kila siku | 18 | 50 |
| Watumiao mara moja kwa juma | 12 | 33 |
| Wasiotumia kabisa | 6 | 17 |
| **Jumla** | **36** | **100** |

Jedwali 4.2 linaonyesha namna walimu hutumia tarakilishi shuleni.

Jedwali 4.2 linaonyesha kuwa ingawa walimu thelathini (30) ama asilimia themanini na tatu (83%) walitumia tarakilishi kufunzia masomo mbalimbali shuleni, walimu wengine, ambao ni sita (6) ama asilimia kumi na saba (17) hawakuzitumia kabisa. Haya ni maelezo ya walimu wakuu, na huku ndiko kuelewa kwao kuhusu iwapo walimu wao walitumia tarakilishi kufunzia masomo shuleni. Walimu wakuu walitoa taarifa ambazo hazikumtosheleza Mtafiti. Ili kuzipata habari kamili na za kujazia zile za walimu wakuu, ilikuwa muhimu kwamba Mtafiti awachunguze walimu wa Kiswahili moja kwa moja. Ni walimu hawa wa Kiswahili ndio walioweza kutoa taarifa za ziada kuhusu matumizi yao ya tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi.

Hata hivyo, ni ukweli wa mambo kwamba walimu hawa wanayumba katika matumizi yao ya tarakilishi. Wao wanadai tu kwamba wanazitumia lakini ujuzi wao unadhihirika kuwa mdogo na hafifu mno. Idadi kubwa ya walimu, ishirini na sita (26) ama asilimia sabini na mbili (72%), hawakuwa na ujuzi maalumu ambao ungewawezesha kujimudu katika kutumia tarakilishi katika kufundisha kwao. Ni walimu kumi (10) ambao walikuwa na ujuzi wa kutumia tarakilishi darasani (tazama Jedwali 4.3).

**Jedwali 4.3 Namna walimu hutumia tarakilishi darasani**

| | Idadi | asilimia |
|---|---|---|
| Walimu wanaotumia tarakilishi darasani | 10 | 28 |
| Walimu wasiotumia tarakilishi darasani | 26 | 72 |
| Jumla | 36 | 100 |

Jedwali 4.3 linaonyesha walimu wanaotumia tarakilishi darasani.

Pia, kuna mabadiliko mengi yanayoibuka kila baada ya kipindi kifupi na ambayo yanahusiana na tarakilishi. Kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa kwamba walimu hawa hawakupatiwa maelekezo ya wakati ili wajimudu vyema katika mchakato mzima wa matumizi ya tarakilishi darasani. Pia, ukosefu wa miundo msingi katika shule nyingi uliweza kuwafifisha katika kutalii na kuimarisha uwezo wao wa matumizi ya tarakilishi.

Halikadhalika, kutokana na majibu ya walimu wakuu, ilionekana hakuna sera maalum inayowaelekeza walimu katika kutumia tarakilishi shuleni. Ndipo idadi ya walimu wanaotumia tarakilishi katika uhalisia wa kufunzia darasani ikawa ni ya chini (tazama Jedwali 4.3). Wale wanaodai kuzitumia, hakika hawazitumii kama inavyodhihirishwa wakati wa maandalizi na katika kuvitazama vipindi vya Kiswahili vikiendeshwa.

Walimu walipoulizwa walipoyapata maarifa ya kutumia tarakilishi walielezea kwamba waliyapata mafunzo hayo walipokuwa katika vyuo vikuu na hata vile vya kufundisha ualimu. Vyuo hivyo ni kama Chuo Kikuu cha Moi, Kenyatta, Maseno, Masinde Muliro nan a Chuo cha Stahashada cha Kagumo (tazama Jedwali 4.4).

**Jedwali 4.4 Namna walimu walipata ujuzi wa tarakilishi**

| | Chuo cha mafunzo | Utokeaji | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1 | Kutoka vyuo vikuu walivyosomea | 34 | 94 |
| 2 | Vyuo vya walimu | 2 | 6 |
| 3 | Vyuo vya tarakilishi | 0 | 0 |
| 4 | Wasiopata mafunzo yoyote | 0 | 0 |
| **5** | **Jumla** | **36** | **100** |

Jedwali 4.4 linaonyesha namna walimu walipata ujuzi wao wa kutumia tarakilishi.

Hata hivyo, ukweli wa mambo ni kuwa mafunzo yanayotolewa katika vyuo mbalimbali huwa hayalengi sana matumizi ya tarakilishi kama wenzo wa kufunzia darasani. Madai haya kwamba walimu hao wana ujuzi wa kutumia tarakilishi ni ghushi. Asilimia sabini na mbili (72%) ya wale walimu walipopatiwa tarakilishi hata hawakutambua kuliko na programu mbalimbali ama hata kuifungua mitambo ya tarakilishi ianze kuchapa kazi (tazama Jedwali 4.3). Hii ina maana kwamba walimu hawajaandaliwa vyema kukabiliana na mchakato wa ufundishaji kwa kutumia teknolojia mpya ya tarakilishi.

Walimu wa Kiswahili walipoulizwa iwapo wao hutumia tarakilishi darasani, walimu kumi (10) ama (28%) walikubali (tazama Jedwali 4.3) Mtafiti alipowauliza shughuli wanazotumia tarakilishi kuzitekelezea shuleni, walitoa maoni tofauti. Kwa mfano, walimu kumi (10) walitumia tarakilishi kutafuta mada za kufunza katika mitandao, kumi na mbili (12) wakawa wakichapishia mitihani, wanane (8) kutayarishia maazimio ya kazi, kumi na sita (16) kuonyeshea video za vitabu vya Fasihi na kumi na tano (15) walifanyia mazoezi ya kupata ujuzi wa kutumia tarakilishi (tazama Jedwali 4.5).

**Jedwali 4.5 Namna tarakilishi hutumiwa na walimu shuleni**

| | Kufanya mazoezi | Mada za kufunza | Kutunga mitihani | Kuandaa maazimio | Kuonyesha video | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi | 15 | 10 | 12 | 8 | 16 | 61 |
| % | 25 | 16 | 20 | 13 | 26 | 100 |

Jedwali 4.5 linaonyesha namna walimu walivyotumia tarakilishi shuleni.

Kadhalika, Mtafiti alitaka kujua hasa ni vipengele vipi ambavyo walimu walivifunza kwa kutumia tarakilishi. Majibu ya hojaji kwa walimu (tazama Kiambatisho cha 2), yalisaidia kuthibitisha maoni ya walimu kama yanavyojitokeza katika Jedwali 4.6

**Jedwali 4.6 Vipengele vilivyofunzwa kwa kutumia tarakilishi**

| **Kipengele** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Fasihi Andishi | 23 | 100 |
| Fasihi Simulizi | 0 | 0 |
| Insha | 0 | 0 |
| Lugha | 0 | 0 |
| **Jumla** | **23** | **100** |

Jedwali 4.6 linaonyesha vipengele vinavofunzwa shuleni kwa kutumia tarakilishi.

Matokeo katika Jedwali 4.6 yanaonyesha kuwa matumizi ya tarakilishi darasani yalijikita tu katika Fasihi Andishihuku Fasihi Simulizi ikipuuzwa. Walimu hasa walieleza kuwa wao hutafuta video za vitabu vya Fasihi Andishina kuwaonyesha wanafunzi kama njia moja ya kuwavutia darasani, kuwapa kumbukumbu ya muda mrefu ya waliyoyasoma na

kubadili muundo wa kufunza. Pia, walikiri kuwa wanafunzi wengi hufurahia mbinu hii ya kufunza kwa kutumia vyombo vya kidijitali kama tarakilishi. Matokeo haya pia yanadhihirisha kuwa walimu wa Kiswahili wanaelewa na wana ujuzi wa kutumia tarakilishi kufunzia vipengele vya Fasihi Andishi.

Haya ni maoni yanayokubaliana na utafiti wa Farrant (k.h.j) uliotamatisha kwa kusema kwamba vifaa vinavyotazamwa na wanafunzi wakati wa masomo huwasaidia kuelewa hali halisi ya mambo. Tatizo ni kuwa walimu hawa hawatumii tarakilishi kufunzia vipengele vya Fasihi Simulizi, lugha na hata insha (tazama Jedwali 4.6). Matokeo haya ni sawa na yale ya walimu wakuu waliosema kuwa ni baadhi tu ya walimu ambao hutumia tarakilishi kufunzia masomo darasani. Mtafiti alipotazama walimu wakiendesha vipindi vyao, pia alithibitisha kuwa walimu hawakutumia tarakilishi kufunza Fasihi Simulizi. Walimu hao hutumia wenzo huu kufunzia vipengele hasa vya Fasihi Andishi na masomo mengine mbali na Kiswahili hasa yale ya sayansi kama Kemia, Bayolojia na Fizikia.

Kwa mujibu wa Jedwali 4.6, ni kipengele cha Fasihi Andishitu ndicho kinachofundishwa kwa wingi kwa kutumia tarakilishi katika shule za upili. Sehemu zingine kama vile Fasihi Simulizi, lugha na insha zilipuuzwa sana. Ufundshaji wa vipengele hivi hukuripotiwa kutumia tarakilishi na walimu waliotafitiwa. Hali hii inajitokeza pia katika utafiti wa Watende (k.h.j) kuhusu matumizi ya nyenzo tofauti katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi. Watende alipata kwamba shule nyingi hazikuwa na nyenzo anuai kama tarakilishi huku walimu wakitumia vitabu tu katika kufundishia somo la Fasihi Simulizi.

Hata hivyo, madai kwamba Fasihi Simulizi haifunzwi kwa kutumia tarakilishi huenda yasiwe ya kweli. Sababu kuu ni kwamba, katika kufundisha mada yoyote, kuna

muingiliano wa vipengele mbalimbali. Kwa kutumia tarakilishi kufundishia Fasihi Andishi, kwa njia moja ama nyingine mwalimu huweza kugusia Fasihi Simulizi. Kuna vipera vya Fasihi Simulizi ambavyo hujitokeza katika Fasihi Andishi. Vipera hivi ni kama nyimbo, semi na michezo ya kuigiza. Wakati wa kufundisha wanafunzi wa Fasihi Andishi kwa kutumia tarakilishi, mwalimu huwa anagusia vipengele hivi vya Fasihi Simulizi. Mwalimu bora nyakati zote huwakumbusha wanafunzi wake kuwa anagusia kipengele fulani cha Fasihi Simulizi huku akifundisha Fasihi Andishi. Kwa hivyo, kwa ujumla hatuwezi kudai tu kwamba Fasihi Simulizi hufunzwa bila matumizi ya tarakilishi.

Kwa mfano, kanda ya Fasihi Andishi ya *Kidagaa Kimemwozea*, ina vipengele vya hadithi ndani ya hadithi, semi kama methali, misemo na nahau pamoja nyimbo ambazo zinaweza kutumiwa kama sehemu ya Fasihi Simulizi. Kanda kama hii inapoonyeshwa kwa kutumia tarakilishi, kwa upande mwingine inaweza kusaidia kuibua vipengele vya Fasihi Simulizi. Hata fanani anayemwigiza *Matuko Weye* katika usemi wake, anaweza kudhihirisha toni mbalimbali ambazo ndizo msingi wa Fasihi Simulizi.

Pia, katika tamthilia ama vitabu vya kuigiza kama *Mashetani* na *Mstahiki meya*, waigizaji wanapocheza sehemu zao tunaweza kuoanisha na Fasihi Simulizi kwa upande wa maigizo. Kipengele cha maigizo ni kimojawapo cha tanzu za Fasihi Andishi nacho huibuliwa vyema kinapoigizwa jukwaani kama ilivyo katika Fasihi Simulizi.

Kulingana na lengo la kwanza la utafiti huu, imebainika kuwa walimu wanaotumia tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi ni asimia kumi tu (10%). Wengine hufundisha vipengele vya Fasihi Simulizi bila kujua huku wakifundisha Fasihi Andishi. Jambo hili linaonyesha aina fulani ya kutofahamu. Iwapo walimu hawa wangeelewa kuwa

wanafundisha vipengele vya Fasihi Simulizi kwa kutumia mawasilisho ya Fasihi Andishi, basi bila shaka wangejifafanua vyema zaidi huku wanafunzi wakifaidika kwa kiasi kikubwa. Jambo hili linasikitisha. Sababu ni kwamba iwapo walimu watatumia tarakilishi kufundishia Fasihi Simulizi basi viwango vya masomo vitaboreshwa katika shule zetu.

Matokeo haya pia yanaelekea kushabihiana na utafiti uliofanywa na Makau (k.h.j) kuhusu matumizi ya tarakilishi darasani. Utafiti wake ulionyesha walimu hawakupendelea matumizi ya tarakilishi katika kufundishia na kuwa walimu hawakupenda kutumia tarakilishi kwa sababu ya ukosefu wa vifaa hivi na ujuzi wa tarakilishi kwa upande wao. Manduku na wenzake (k.h.j) walijaribu kutoa ufafanuzi wa suala hili kwa kulaumu ukosefu wa nguvu za umeme katika shule za upili.

Kutokana na hali hii, si ajabu basi kuona uwepo wa matumizi haba ya tarakilishi katika shule za upili. Hali hii inakuwa mbaya zaidi hasa tunapoangazia ufundishaji wa Fasihi Simulizi kwa kutumia tarakilishi.

Walimu na wakuu wa shule hawajaichangamkia sana mbinu hii mpya ya ufundishaji. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kuwa wao hawajakubali kabisa matumizi ya tarakilishi. Rogers (k.h.j) katika nadharia yake ya NUMT anasema kuwa huenda teknolojia mpya inayozinduliwa ikakataliwa na wapokezi wake iwapo haionyeshi faida kwao. Ukweli ni kwamba teknolojia hii ina faida. Hali hii ya kutoitumia kwa kiasi kikubwa inazua tetesi ama kuna sababu zingine nyingi zinazosababisha haya kutokea kama vile ukosefu wa pesa, mafundisho na nishati shuleni. Haya yakitekelezwa bila shaka walimu, wanafunzi na wadau wengine wataichangamkia mbinu hii. Wao wataikubali na basi kuitumia kikamilifu kufunzia Fasihi Simulizi.

## 4.3 Maandalizi ya vipindi vya Fasihi Simulizi kwa kushirikisha tarakilishi

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kuchunguza namna walimu huandaa vipindi vya Fasihi Simulizi kwa kutumia tarakilishi. Mtafiti aliomba kuangalia maandalizi ya vipindi kabla ya kuandamana na walimu darasani ili kuona namna ambavyo wangeendesha vipindi vyao. Swali la 9 C katika Hojaji ya walimu ilimwongoza Mtafiti kupata majibu yaliyofaa (tazama Kiambatisho cha 2).

Maeneo yaliyohusishwa katika maandalizi ya vipindi yalikuwa kama ifuatavyo: namna walimu walitayarisha maazimio ya kazi, maandalio ya masomo, pamoja na nukuu za masomo kwa ajili ya wanafunzi. Mtafiti pia alilenga kuchunguza maandalizi ya vifaa vya kufunzia Fasihi Simulizi, madarasa ambamo wanafunzi walipangiwa kufundishiwa vipindi hivyo, matayarisho ya nishati mbadala iwapo nguvu za umeme zingetatiza, kuwaandaa wanafunzi pamoja na uhusishwaji wa walimu wenye ujuzi na tajiriba ya tarakilishi. Walimu hawa wangekuwa wa kutoa msaada mkubwa iwapo mitambo ya tarakilishi ingetatiza ama kuonyesha hitilafu yoyote ile na ambayo mwalimu wa Kiswahili hangeelewa jinsi ya kutatua.

### 4.3.1 Maazimio ya kazi

Mtafiti alitumia mbinu ya utazamaji katika kuchunguza namna walimu walijiandaa kufundisha vipindi vyao. Kwanza alitaka kuona maazimio yao ya kazi. Walimu wote walimkabidhi nakala zao za maazimio ya kazi. Baada ya kuzipitia kwa kina, Mtafiti aligundua kwamba walimu wote thelathini na sita (36) ambao ni 100% hawakuhusisha wenzo wa kutumia tarakilishi katika vipindi vyao. Mfano wa azimio la kazi la juma moja kutoka shule ya wasichana ya Mtakatifu Agostino Lukhuna liko katika Kiambatisho cha 9. Mfano huu ni sawia na maazimio ya kazi katika shule zingine zilizofanyiwa utafiti.

Katika maazimio haya, ni dhahiri kuwa walimu hawakuhusisha tarakilishi kama kimojawapo cha vifaa vya kutumia katika kufundisha kwao bali waliegemea kwa vifaa asilia kama ubao, chaki na chati pamoja na mbinu zingine za kufundishia.

Hali hii inaonyesha udhaifu uliopo katika maandalizi ya vipindi vya Kiswahili na hasa vile vya Fasihi Simulizi. Iwapo walimu hawatajumuisha vifaa fulani katika maazimio yao ya kazi basi huenda ikawa vigumu sana kuwashawishi walimu wakuu kwamba wangetaka kuvitumia vifaa hivyo darasani. Labda hii ndiyo sababu baadhi ya walimu wakuu hawajanunua tarakilishi za kutosha shuleni mwao pamoja na kuwafadhili walimu kwenda katika semina na warsha.  Semina za aina hii huwa mwafaka katika kuboresha ujuzi wa walimu wa kutumia tarakilishi.

### 4.3.2 Mpangilio wa somo

Kipengele cha pili ambacho kilitazamwa katika maandalizi kilikuwa mpangilio wa somo. Hiki ni chombo muhimu katika kumwongoza mwalimu kutimiza majukumu yake. Mpangilio wa somo humwezesha mwalimu kuwasilisha somo lake hatua kwa hatua kwa njia ya kitaaluma. Mwalimu anayekosa mpangilio wa somo huweza kutatizika akiwa darasani. Kwa hivyo, Mtafiti alikitazama chombo hiki kwa walimu thelathini na sita (36) aliowachunguza. Matokeo yalikuwa kwamba hapana mwalimu hata mmoja kati yao aliyeandaa mpangilio huu kwa ajili ya kufundishia Fasihi Simulizi. Sababu walizozitoa ni kwamba vipindi walivyo navyo ni vingi sana (kwa wastani vipindi 24 kwa juma moja) na inakuwa vigumu kwao kuandaa maandalio ya masomo kwa vipindi vyote hivyo. Wao walidai kwamba muradi walikuwa na nukuu za masomo basi kazi ingefanyika vyema tu. Kwa upande mwingine walimu hawa hawakutaka ukweli huu uwekwe wazi kwa maana ni hitaji mojawapo la Wizara ya Elimu kwamba walimu wote waandae maandalio ya

masomo kwa vipindi vyote ambavyo wanavifundisha. Hata hivyo, iwapo walimu watapunguziwa idadi ya vipindi basi wataweza kuandaa masomo vyema na hasa maandalio ya vipindi vya Fasihi Simulizi ili wawafaidi wanafunzi pakubwa.

### 4.3.3 Nukuu za masomo

Kipengele cha tatu kilikuwa nukuu za masomo. Haya ni makala maalumu ambayo mwalimu huyaandaa ili kuwapatia wanafunzi wakati wa kipindi. Mtafiti basi aliwauliza walimu wamwonyeshe nukuu hizi. Walimu wote thelathini na sita (36) ama 100% waliotafitiwa walikuwa nazo ingawa nyingi ya nukuu hizo hazikuandaliwa kwa kutumia tarakilishi (tazama Jedwali 4.7). Walimu kumi na watano (15) ambao ni asilimia arobaini na mbili (42%) ya walimu walitumia tarakilishi katika kuandaa nukuu zao za masomo. Hali hii iliwasaidia katika kuwasilisha mada zao vizuri licha ya kwamba hawakuwa na maandalio ya masomo.

**Jedwali 4.7 Idadi ya walimu waliotumia tarakilishi kuandaa nukuu.**

| | Idadi | % |
|---|---|---|
| Walimu waliotumia tarakilishi | 15 | 42 |
| Walimu wasiotumia tarakilishi | 21 | 58 |

Jedwali 4.7 linaonyesha walimu waliotumia tarakilishi kuandaa nukuu za masomo

Jambo hili linatia moyo sana kwamba baadhi ya walimu licha ya kwamba hawakuzitumia tarakilishi darasani lakini ziliwafaa katika kuandaa nukuu zao ambazo zilionekana nadhifu zaidi na za kuvutia. Nukuu hizo ziliweza kuamsha ari ya kusoma miongoni mwa

wanafunzi. Pia, nukuu hizo zilisaidia sana kuokoa wakati huku wanafunzi wakikabidhiwa nakala za nukuu hizo.

Hoja nyingine aliyoitazama Mtafiti kabla ya vipindi darasani ilikuwa uwepo wa madarasa ya kufundishia masomo kwa kutumia tarakilishi. Mtafiti aliona kwamba ilikuwa muhimu kuyachunguza madarasa ambamo mngetumiwa kufundishia vipindi kwa kutumia tarakilishi. Hili lilikuwa muhimu kwa baadhi ya shule kwani umeme haukuwemo katika madarasa yote. Mtafiti basi alitambua madarasa hayo kwa kusaidiwa na waelekezi wa shule. Hata hivyo, kwa maana walimu hawakutumia tarakilishi kufundishia Fasihi Simulizi, basi wanafunzi walibaki katika madarasa yao. Hoja hii iliendana na matayarisho ya vyumba maalumu vilivyo na umeme kwa baadhi ya shule zisizo na umeme katika maeneo yote ya utafiti. Kwa hivyo Mtafiti ilibidi atambue vyumba ambavyo vilikuwa na umeme kabla ya kwenda kuonana na walimu wa Kiswahili.

### 4.3.4 Maandalizi ya wanafunzi na walimu wasaidizi

Hatimaye Mtafiti alitaka kuchunguza namna walimu wa Kiswahili walivyowatayarisha wanafunzi pamoja na walimu wenye tajiriba ya tarakilishi kabla ya vipindi vyao kufika. Hili lilikuwa muhimu kwa sababu wanafunzi wakijua kwamba watafundishwa kwa kutumia kifaa cha kidijitali wao huchangamka sana. Wanafunzi wengine hufanya haraka ya kufika katika vyumba maalumu vya tarakilishi. Nao walimu wenye tajiriba ya tarakilishi huweza kumnufaisha mwalimu wakati anapokwama ama kutatizika na mitambo.

Katika hali hii, Mtafiti alitarajia kwamba vipindi vitakuwa bora sana lakini walimu wakashindwa kutumia tarakilishi kufundishia Fasihi Simulizi. Hali hii huenda ilitokana na

walimu kukosa tajiriba ya tarakilishi na pia wao kutotilia maanani umuhimu wa matumizi ya tarakilishi katika kufundishia wanafunzi. Pia, Wizara ya Elimu haijatoa mwongozo dhahiri wa ni kwa namna gani wenzo wa tarakilishi unafaa kutumiwa katika kufundishia masomo mbalimbali shuleni.

Kutokana na utazamaji wa maandalizi ya vipindi, Mtafiti alipata kuwa walimu hawakuwa tayari kutumia tarakilishi katika kufundishia Fasihi Simulizi. Hii ina maana kuwa walimu hao hawakuwa na nia ya kutumia au walikosa ujuzi wa kutumia tarakilishi ingawa awali walikubali kuwa walikuwa na ujuzi wa kutosha na hata wengine wakiwa wanazitumia.

Mtafiti alipata kwamba walimu walihusisha nyenzo zingine kama vitabu, picha, michoro na ubao na kukwepa matumizi ya teknolojia za kisasa kama tarakilishi. Katika mahojiano (tazama Kiambatisho 3 na 4), walimu walikiri kuwa hawakuwa na ujuzi wa kutumia tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi. Pia, hakuna mafunzo yaliyoandaliwa katika kipengele hiki ili wayatumie darasani. Walilalamikia muda mchache wa kutumia teknolojia kwani vipindi na mada za kushughulikiwa zilikuwa nyingi.

Nadharia ya Rogers (k.h.j) inaeleza kuwa iwapo wahusika ama wapokezi wa teknolojia mpya hawataikubali basi huenda ikawa vigumu kutumika. Walimu hawajaipokea vyema tarakilishi kama wenzo wa kisasa wa kufundishia hasa somo la Fasihi Simulizi. Labda wanaangazia tu ugumu wa kupatikana kwake na matatizo yanayoambatana na matumizi yake na hivyo basi kuipuuza. Walimu hawa wanashindwa kutambua umbali teknolojia hii mpya inapoweza kuwafikisha katika uwasilishaji wa matini zao kwa wanafunzi. Wanafunzi wana uwezo mkubwa wa kuipokea na kuichangamkia teknolojia ya tarakilishi muradi tu walimu wataitumia.

### 4.4 Changamoto katika matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kuonyesha changamoto zinazowakumba walimu wa Kiswahili katika kutumia tarakilishi kama kifaa cha kufundishia Fasihi Simulizi. Kupitia kwa hojaji ya walimu wakuu (Kiambatisho 5) na mahojiano na walimu (Kiambatisho 3), Mtafiti alipata maoni ya wasailiwa. Jedwali 4.8 linaonyesha baadhi ya changamoto za walimu pamoja na walimu wakuu katika kutumia tarakilishi kufundishia masomo mbalimbali shuleni na hasa somo la Fasihi Simulizi.

**Jedwali 4.8 Changamoto katika harakati za kutumia tarakilishi**

| **Changamoto** | **Idadi** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Uhaba wa tarakilishi | 19 | 35 |
| Ukosefu wa muda | 17 | 31 |
| Ukosefu wa ujuzi | 10 | 19 |
| Matatizo ya umeme | 4 | 7 |
| Mitambo kuharibika | 2 | 4 |
| Ukosefu wa mada za Fasihi Simulizi katika mfumo wa kidijitali. | 2 | 4 |
| **Jumla** | **54** | **100** |

Jedwali 4.8 linaonyesha changamoto za kutumia tarakilishi shuleni.

#### 4.4.1 Uhaba wa tarakilishi

Jedwali 4.8 linaonyesha kuwa walimu kumi na tisa (19) ambao ni asilimia thelathini na tano (35%) ya walimu walikiri kuwepo kwa uhaba wa tarakilishi katika shule zao. Walimu walisema kuwa idadi ya tarakilishi ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi. Shule hazikuwa na projekta ambazo zingesaidia walimu kutumia hata

tarakilishi moja tu. Wakati mwingi tarakilishi zilizoko shuleni zingetumiwa kwa shughuli za ofisi na kufunza somo la tarakilishi. Basi walimu hawakupata nafasi kuzitumia. Hali hii ni kweli kwa maana shule hizi bado zinajijenga na mara kwa mara hazijaonyesha ukwamuzi wa kutosha. Hata hivyo, kwa vile shule zilizotafitiwa ni zile teule, inaaminika kuwa serikali imezipatia vifaa mbalimbali vya kufundishia zikiwemo tarakilishi. Kwa hivyo uhaba huu ambao uliripotiwa kwa kiasi kikubwa huweza ukawa ulitokana na misaada mingine ambayo huwa ni ghushi. Katika baadhi ya shule kulikuwepo tarakilishi lakini mitambo yenyewe ilikuwa ishapitwa na wakati na isiyofaa kwa wakati huu.

Ni jambo la muhimu kusema kwamba baadhi ya watoao misaada huzitumia shule kama maeneo ya kutupa vifaa vyao duni vilivyopitwa na wakati. Aghalabu wao husema kwamba ni msaada ama wengine wakifanya biashara haramu. Pia, walimu na hasa walimu wakuu wengine hawana umakini katika kuvikagua vifaa vyovyote vinavyoletwa shuleni na wafadhili ama wanavyovinunua ili viwe vinavyotosheleza mahitaji ya wakati. Huenda pia Wizara ya Elimu haijatambua kwamba kizazi cha sasa kina vijana ambao wengi hutambua ufanyakazi wa mitambo ya kidijitali. Basi misaada ya mitambo hii inapoletwa shuleni lazima iwe inayoendana na mahitaji ya wakati. Jambo la ajabu ni kwamba shule takribani zote zilikuwa na walimu walioelewa tarakilishi. Hata hivyo, wengi wa walimu wakuu huwa hawawahusishi walimu hawa katika ununuzi wa vifaa hivi vya tarakilishi. Vitendo hivi ndivyo husababisha ukosefu ama urundikaji wa mitambo ghushi shuleni ambayo hutumiwa tu kuwahadaa wageni na wazazi.

### 4.4.2 Ufupi wa wakati

Walimu kumi na tisa (19) ambao ni asilimia thelathini na moja (31%) ya wasailiwa waliripoti kwamba hawakutumia tarakilishi kwa maana ya ukosefu wa wakati wa

kutosha. Walimu walilalamikia muda mchache ilhali wakiwa na mada nyingi za kushughulikiwa katika somo la Kiswahili. Walimu wa Kiswahili pia walifundisha masomo mengine kwa hivyo hawakuwa na muda wa kuandaa vipindi vinavyoshirikisha vifaa tofauti. Iliibuka pia kwamba mfumo wa elimu ulitilia mkazo mitihani kwa hivyo walimu hutumia muda wao mwingi kuandaa wanafunzi kwa mitihani. Mbinu na vifaa vya kufunza havipewi tena umuhimu unaostahili. Walimu basi hupuuza matumizi mwafaka ya vifaa hivi.

Walimu hao walidai kuwa kipindi cha Kiswahili, kama vilivyo vipindi vingine, ni kifupi sana yaani dakika arobaini (40). Walimu hao walisema kuwa ni vigumu kwao kuandaa kipindi cha tarakilishi katika muda huo mfupi. Walipendekeza kuwa angaa mara moja kwa juma vipindi viwili viunganishwe ili kuwe na dakika themanini (80) za matumizi ya tarakilishi kwa kila darasa.

Mbali na kwamba dai hili ni kweli, lakini ni muhimu ifahamike kuwa mwalimu aliyejipanga sawasawa ana uwezo mkubwa wa kuwasilisha kazi yake kwa kutumia tarakilishi katika dakika hizo arobaini (40). Kwa mfano, mwalimu atahifadhi kazi yake katika kinuruweo na afikapo darasani hatapoteza wakati wowote ila ataanza kuwafundisha wanafunzi wake. Picha na maandishi yatarushwa ukutani huku wanafunzi wakielekezwa. Isitoshe, walimu walio na ujuzi na utambuzi wa haraka wana uwezo wa kuzigawa mada kama hizo katika vipindi vifupi vifupi bila tatizo lolote. Hali hii husaidia sana kuokoa wakati.

Sifa moja kuu na ambayo inachochea matumizi ya tarakilishi kama wenzo wa kufundishia darasani ni kwamba huokoa muda. Kwa hivyo walimu waliotoa madai haya huenda

hawakusema kweli ama wao hawana ujuzi wa kutumia tarakilishi. Lazima walimu wafanye maandalizi ya mapema na wafanyavyo hivyo huku wakitumia kifaa kama vile kinuruweo, bila shaka wataokoa muda na uwasilishaji wao wa kazi utakuwa bora zaidi.

### 4.4.3 Ukosefu wa ujuzi wa kutumia tarakilishi

Nao walimu kumi (10) ambao ni asilimia kumi na tisa (19%) ya wasailiwa waliripoti kukosa ujuzi wa kutumia tarakilishi darasani wanapofunza. Pia, baadhi ya tarakilishi ni za zamani, hazina teknolojia za kisasa na hata huharibika kila mara. Walimu walisema hizi tarakilishi mbovu huwakatisha tamaa kujaribu kuzitumia darasani ikichukuliwa kwamba idadi kubwa ya walimu hawana ujuzi wa kurekebisha mitambo hiyo. Pia inakuwa aibu kutumia mitambo iliyozeeka na kupitwa na wakati ilhali baadhi ya wanafunzi wanamiliki mitambo ya kisasa hasa wakiwa nyumbani. Wao huwasikitikia sana walimu wanaobabaika kutumia mitambo hiyo iliyopitwa na wakati. Labda hii ni mojawapo ya sababu zinazowahofisha walimu wengine kutumia tarakilishi za sampuli hii darasani.

Walimu hutumia teknolojia hii kufanya tafiti na mawasiliano ya kibinafsi. Huenda huku kukosa ujuzi kunachangia walimu kukwepa hii teknolojia wakati wa kufunza darasani. Utafiti wa Wanjala, Khaemba na Mukwa (k.h.j) unaonyesha kuwa walimu wengi hawakuwa na ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa kama tarakilishi. Ingawa walimu katika utafiti huu walikiri kuwa walikuwa weledi wa tarakilishi, ajabu ni kwamba takribani wote waliepuka matumizi ya tarakilishi katika kufundishia darasani na hasa Fasihi Simulizi.

Hali hii inaweza kutokana na walimu hawa kushindwa kuboresha ujuzi wao wa tarakilishi kila mara. Wengi wao huenda baada ya kupata mafunzo haba wakiwa vyuoni, kama walivyodai, walisahau kufanya mazoezi na kuongeza maarifa mapya na ambayo

hubadilika kila mara. Walimu sampuli hii huwa washatosheka katika matumizi ya mbinu za kawaida za kufundishia kama vile maelezo, mihadhara n.k. Aghalabu matumizi ya tarakilishi, mbali na kwamba yana manufaa mengi, lakini humhitaji mwalimu kujitolea sana ili afanye mazoezi ya kina kabla ya kuwa mweledi wake. Walimu wazembe watashindwa kuitumia mbinu hii ya tarakilishi kwa kukosa mazoezi ya kila mara.

Hali hii ya walimu kutoyaenzi matumizi ya tarakilishi katika kufundishia Fasihi Simulizi inaelekea kukubaliana na nadharia ya Rogers (k.h.j) ya Ukubalifu na Matumizi ya Teknolojia (NUMT). Rogers anasema kuwa teknolojia mbalimbali hupitia hatua kadha ndiposa ikubalike na kisha kutumika kwa wingi. Inaelekea kuwa huu ni wakati tu wa mpito ambapo tarakilishi inapitia hatua hizi. Baada ya muda fulani, huku wanaoienzi tarakilishi wakipiga hatua kubwa mbele kimaendeleo, bila shaka wale wafanyao mambo polepole wataufuata mkondo huo wa mabadiliko. Kilicho cha muhimu ni kuwa teknolojia ya tarakilishi inaendelea kufanya maendeleo ya hali ya juu kila siku. Katika muktadha huu, ni wazi kuwa umuhimu wake pia unadhihirika. Ukweli huu wa ubora wa tarakilishi katika nyanja zote za maisha utawalazimisha walimu kuuona uzuri wa matumizi ya tarakilishi katika kufundishia Fasihi Simulizi darasani. Punde idadi kubwa ya walimu hawa itatambua ubora wa tarakilishi na basi kuzitumia sio tu katika kufunzia vipengele vya Kiswahili bali masomo yote yaliyomo katika mtaala wa elimu nchini Kenya.

Hata hivyo, ni vyema ifahamike kuwa uzembe kazini ndio unaofifisha matokeo mema ya wanafunzi wakiwa shuleni. Kwa hivyo, ni muhimu walimu wachukue hatua ya haraka kufanya maandalizi ya mapema wanapojiandaa kuendesha vipindi vyao. Wakifaulu kufanya hivi, bila shaka ujuzi wao wa kutumia tarakilishi utaimarika na kwa haraka matokeo ya wanafunzi katika Fasihi Simulizi na masomo mengine yatakuwa bora.

### 4.4.4 Matatizo ya umeme

Matatizo ya umeme yaliripotiwa na walimu wanne (4) ama asilimia saba (7%) ya walimu wote. Wao walisema matatizo ya umeme yalizua changamoto kubwa. Ingawa serikali imejitahidi kusambaza umeme kwa shule zote zaupili katika kaunti ya Bungoma, utafiti huu ulithibitisha kuwa shule zingine zinakumbwa na matatizo makubwa ya umeme. Shule kumi kati ya kumi na nane zilizotafitiwa zilikuwa na umeme katika ofisi za utawala pekee. Kwa vile tarakilishi hutumia umeme, walimu katika shule hizo walishindwa kutumia teknolojia kwa sababu hawakuwa na njia mbadala. Kwa mfano, utafiti wa Manduku, Kosgey na Sang (k.h.j) kuhusu matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji nchini Kenya ulionyesha kuwa jambo hili halijatekelezwa kwa sababu ya ukosefu wa umeme katika shule nyingi na uhaba wa tarakilishi.

Shule zingine zina umeme lakini hukatizwa mara kwa mara kwa sababu ya matatizo ya mitambo. Wakati mwingine umeme unaweza kupotea kwa zaidi ya siku moja. Hali hii huweza kutokea wakati mwalimu anatumia tarakilishi darasani. Hili humfisha moyo na kumfanya kuepuka kutumia teknolojia ya tarakilishi darasani.

### 4.4.5 Ukosefu wa mada za Fasihi Simulizi

Mtafiti alipata changamoto nyingine ambayo ilikuwa ukosefu wa mada za Fasihi Simulizi katika mfumo wa dijitali. Walimu wawili (2) ama asilimia nne (4%) ya wasailiwa walisema kuwa kando na video za vitabu vya Fasihi, wataalam wa elimu hawajawaandalia mada za kidijitali ambazo wangetumia kufunzia Fasihi Simulizi kama walivyofanya katika masomo mengine. Hata hivyo, dai hili halina msingi kwa maana walimu ndio hao wataalamu wenyewe. Inabidi walimu wawe wabunifu kiasi kwamba wawezeshwe kujiundia video na makala ambayo watayatumia darasani. Kuandaa vipindi

vya kinuruweo hakuhitaji kununua programu maalumu kwa ajili yake. Kilicho cha muhimu ni walimu hawa kuhudhuria warsha na semina zinazofundisha matumizi ya tarakilishi. Pia, walimu wawe tayari kujifunza wenyewe kwa maana ulimwengu unazidi kubadilika na kuhitaji mambo mageni kila siku. Yule asiyejifunza teknolojia hii mpya na kuitumia kikamilifu huenda hivi karibuni asiwe wa maana yoyote kama mwalimu.

Kutokana na hojaji ya walimu wakuu (tazama Kiambatisho 5), Mtafiti alipata kwamba shule nyingi hazina fedha za kutosha kununua vifaa vya kufunzia zikiwemo tarakilishi. Ni fedha chache tu ambazo hutengwa kwa shughuli hii huku wasimamizi wa shule wakiandaa bajeti kubwa kila mwaka ilhali wana fedha kidogo.

### 4.4.6 Fikra za kutosheleka kwa walimu

Tatizo lingine walilotaja walimu wakuu ni fikra za baadhi ya walimu kuwa wao wana ujuzi wa kutosha na hawatumii mbinu mbadala kufunzia. Walimu hawa walikuwa hasa wa umri wa zaidi ya miaka hamsini (50). Wao hawakufanya juhudi zozote kutumia tarakilishi katika kufundishia Fasihi Simulizi. Hata hivyo, inawahitaji walimu hawa kutambua kwamba maarifa hupanuka kila siku. Yeyote anayeegemea upande wa kutotaka kupanua kiwango chake cha elimu basi huwa hana nafasi tena katika jamii ya sasa. Walimu hawana budi kujizatiti katika kutumia teknolojia mpya ili wayahamishe maarifa waliyo nayo kwa wanafunzi ambao wamewaaminia kuwatunza. Ni sharti Kiswahili kifundishwe kwa kutumia tarakilishi na hasa Fasihi Simulizi ili pawepo na ukwamuzi wa alama za mitihani.

Mfumo wa elimu ambao una mada nyingi za kushughulikiwa katika muda mfupi pia ulichangia walimu kukwepa kutumia tarakilishi. Walimu wakuu walisema kuwa walimu

wao hutumia muda mwingi kufunza mada zilizopendekezwa na kuwaandaa wanafunzi kufanya mitihani ya kitaifa. Basi wengi walikosa nafasi ya kushirikisha mbinu ya tarakilishi na teknolojia tofauti katika ufundishaji wao.

Hata hivyo walimu wakuu na walimu wa Kiswahili walioshiriki katika utafiti huu walikubali kwamba tarakilishi ni wenzo muhimu wa kutumia katika ufundishaji. Kifaa hiki kinaweza kuboresha mazingira ya darasani, kufurahisha wanafunzi na kunoa akili zao. Tarakilishi huweza kuleta uhalisia wa aina yake darasani na kuwasaidia wanafunzi na walimu kutafiti mada tofauti. Walimu wakuu walipendekeza kuwa warsha za kila mara zikiandaliwa zitawafaa walimu kupata ujuzi wa kutumia teknolojia mpya kama tarakilishi ili kuboresha ufunzaji wao.

### 4.5 Mbinu mbadala wanazotumia walimu kufunzia Fasihi Simulizi

Lengo la nne la utafiti huu lilikuwa kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa shule za upili za kaunti ya Bungoma katika kufundishia Fasihi Simulizi. Katika kutimiza wajibu huu, Mtafiti aliwauliza walimu wote thelathini na sita (36) kuhusu mbinu wanazozitumia katika kufundishia Fasihi Simulizi. Wasailiwa walisema kwamba wao walitumia mbinu zifuatazo katika kufundishia Fasihi Simulizi: maelezo, maswali na majibu, majadiliano, maigizo, mihadhara, wageni waalikwa, kazi mradi, kanda za video pamoja na mbinu ya ziara. Matumizi ya mbinu hizi yameonyeshwa katika Jedwali 4.9. Kijumla, wasailiwa walitumia mbinu hizi mara mia moja na mbili (102) kama zinavyoonyeshwa katika Jedwali 4.9.

### 4.5.1 Maoni ya wasailiwa

Kupitia kwa hojaji na mahojiano ya walimu (tazama Kiambatisho 1, swali la 10 na Kiambatisho 3, swali la 11), Mtafiti alipata maoni ya wasailiwa yaliyolijibu swali hili. Jedwali 4.9 linaonyesha baadhi ya mbinu za kufundishia ambazo walimu wa Fasihi Simulizi walizitumia wakiwa darasani.

**Jedwali 4.9 Mbinu za kufundishia ambazo walimu wa Fasihi Simulizi walizitumia**.

| Mbinu za kufundishia | Walimu waliotumia | Asilimia |
|---|---|---|
| Maelezo | 20 | 20% |
| Maswali na majibu | 25 | 24% |
| Majadiliano | 18 | 17% |
| Maigizo | 06 | 6% |
| Mhadhara | 04 | 4% |
| Wageni waalikwa | 05 | 5% |
| Kazi mradi | 06 | 6% |
| Kanda video | 15 | 15% |
| Ziara za nyanjani | 03 | 3% |
| **JUMLA** | **102** | **100**% |

Jedwali 4.9 linaonyesha mbinu ambazo walimu hutumia kufundishia Fasihi Simulizi.

### 4.5.2 Mbinu ya kuuliza na kujibu maswali

Wanjala na Kavoi (2013) wanasema kuwa mbinu ya maswali na majibu inaweza kutumiwa kufunzia vidato vyote shuleni. Mbinu hii ilitumiwa na wasailiwa ishirini na watano (25) ikiwa ndiyo ilichaguliwa na wasailiwa wengi zaidi. Idadi hii iliwakilisha asilimia ishirini na nne (24%) ya matumizi yote (tazama Jedwali 4.9). Matumizi yake

hutokea wakati mwalimu akifundisha huku akiwauliza wanafunzi maswali akiwapima iwapo wanaelewa kinachofundishwa. Mwanzoni, wanafunzi huyajibu maswali hayo. Wanafunzi wanaoshindwa kuyajibu maswali hayo huelekezwa na mwalimu. Wanafunzi pia huruhusiwa kuuliza maswali ambayo hujibiwa na wanafunzi wenzao ama kujibiwa na mwalimu. Hii ni mbinu mwafaka ambayo imetumiwa kwa muda mrefu mpaka sasa. Hata hivyo, ni bora itikitumiwa na muungano wa mbinu zingine za kufundishia ikiwemo video na tarakilishi.

### 4.5.3 Mbinu ya Maelezo

Mbinu nyingine iliyotumiwa sana na wasailiwa katika kufundishia Fasihi Simulizi ilikuwa mbinu ya maelezo. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) maelezo ni maneno yanayofahamisha kitu au habari fulani. Wasailiwa ishirini (20) walikiri kutumia mbinu ya maelezo. Idadi hii ni sawa na asilimia ishirini (20%). Hii ina maana kuwa ni wasailiwa wengi tu ambao huitumia mbinu hii. Wao wakiwa darasani, huwafundisha wanafunzi kwa kuwatolea maelezo kuhusu mada za Fasihi Simulizi kama vile hadithi, semi na nyimbo. Huzifafanua hadithi, maana yake, vipera vyake, sifa, umuhimu wake katika jamii n.k. Mwalimu ndiye huwa mjuzi na kielekezi darasani. Ingawa wanafunzi hufahamu mada barabara lakini mbinu hii inahitajika kutumiwa pamoja na mbinu zingine kama maswali na majibu ili kuboresha ufundishaji wa mwalimu. Wanafunzi wa sasa hawatosheki tu na maelezo kwani wao huhitaji vyombo vya kisasa kama tarakilishi ili wasisimke wakiwa darasani huku wakiepuka uchovu unaowalemea baada ya muda mrefu wa kukaa darasani.

### 4.5.4 Majadiliano

Wasailiwa kumi na wanane (18) walijibu kwamba wao hutumia mbinu ya majadiliano kufunzia Fasihi Simulizi. Idadi hii inawakilisha asilimia kumi na saba (17%). *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) inafafanua majadiliano kama mazungumzo yanayohusu watu zaidi ya mmoja ambao hubadilishana mawazo kuhusu mada moja. Majadiliano ni mwafaka katika madarasa mengi na walimu huvutiwa nayo. Mbinu hii inatumika sana katika kufundishia mada kama umuhimu wa vipengele vya Fasihi Simulizi, mchango wa vipengele hivyo katika jamii na sifa za vipera mbalimbali vya Fasihi Simulizi. Walimu huichangamkia sana mbinu ya majadiliano kwa sababu maandalizi ya vipindi hayahitaji kazi kubwa kama ilivyo katika mbinu zingine kama kazi mradi na mbinu ya ziara.

### 4.5.5 Kanda na santuri

Mbinu ya kanda na santuri ilichaguliwa na wasailiwa kumi na watano (15). Kwa ujumla, idadi hii iliwakilisha asilimia kumi na tano (15%). Mbinu hii imetumika kwa muda mrefu sasa. Mwanzoni walimu walitumia kanda za sauti na hatimayi zikazinduliwa zile za video. Hizi kanda huleta mazingira hai darasani na kuwawezesha wanafunzi kuelewa mada kwa urahisi. Vipera vya Fasihi Simulizi kama vile nyimbo, sherehe za tohara na miviga huweza kutazamwa na wanafunzi wakiwa darasani. Katika njia moja ama nyingine, matumizi ya mbinu hii ya video inashabihiana sana na ile ya tarakilishi. Hata hivyo, matumizi ya tarakilishi ni ya kiwango cha juu huku mada zikiweza kupakuliwa kutoka mtandaoni wakati wowote bila tatizo. Mbinu hii ni nzuri na inafaa walimu waitumie sana katika kufunzia Fasihi Simulizi. Wale waitumiao pamoja na tarakilishi watakuwa na uhakika wa kupata ufanisi katika ufundishaji wao.

### 4.5.6 Mbinu ya maigizo

Kwa mujibu wa Matei (2012) maigizo ni drama ikiwa na maana ya mazungumzo yanayoambatana na matendo. Katika maigizo wahusika waigizaji huigiza tabia, maneno na matendo ya watu wengine katika jamii kwa nia ya kuburudisha na kupitisha ujumbe fulani. Mbinu hii ya ufundishaji ilitumiwa na wasailiwa sita (6), idadi hii ikiwakilisha asilimia sita (6%). Aghalabu matumizi yake huwahitaji waigizaji wenye tajiriba kubwa. Ukosefu wao unawafanya walimu wengine kuyapuuza matumizi yake. Hata hivyo, hii ni mbinu nzuri ambayo inapotumika husaidia sana kuhifadhi kumbukumbu ya wanafunzi kwa muda mrefu. Ingawa mbinu hii inaonyesha utata wa kuitumia, lakini mwalimu anaweza kuwatayarisha baadhi ya wanafunzi wake kufanya maigizo mafupi ambayo yanaweza kukuzwa baadaye. Pia, kuna vikundi vingi tu ambavyo vinaweza kualikwa shuleni na kuwaigizia wanafunzi vipera mbalimbali vya Fasihi Simulizi. Vikundi hivi ni kama *Jicho 4* na *The State Productions* kutoka Nairobi. Walimu walioitikia kuitumia mbinu hii wote walikiri kuvialika vikundi hivi katika shule zao.

### 4.5.7 Mbinu ya mhadhara

Mhadhara, kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (k.h.j) ni maelezo juu ya mada fulani yanayotolewa mbele ya watu ama wanafunzi, hasa katika vyuo vya juu kwa ajili ya kufundisha. Mbinu hii ya ufundishaji ilitumiwa na walimu wanne (4) ama asilimia nne (4%) tu. Utokeaji huu hafifu unaweza kuwa kwa sababu ni mbinu isiyowafaa sana wanafunzi wa sekondari. Hata hivyo, kunaweza kuwa na hitaji la kuitumia mbinu hii wakati mwalimu akiwa amezidiwa na idadi kubwa ya wanafunzi. Hali hii inadhihirika sana wakati huu katika shule nyingi nchini. Mbinu ya mhadhara inapotumiwa katika vyuo vikuu, huwa ni kwa sababu ya uchache wa wahadhiri. Hivyo basi, idadi kubwa ya

wanafunzi wanaosajiliwa katika shule za upili ndiyo iliyochangia kuibuka kwa mbinu hii. Hata hivyo, ni vyema kwamba mbinu hii ikitumiwa pawepo na maandalizi mazuri kama udumishaji wa nidhamu huku mbinu zingine kama maelezo na maswali na majibu zikitumiwa wakati mmoja.

### 4.5.8 Mbinu ya wageni waalikwa

Mbinu ya wageni waalikwa ilichaguliwa kutumiwa na walimu wanne (4). Jedwali 4.9 linaonyesha kwamba idadi hii ya wasailiwa iliwakilisha asilimia tano (5%). Wanjala na Kavoi (k.h.j) wanadai kuwa wageni waalikwa ni wataalamu katika tasnia fulani. Hawa ni watu walio na tajiriba na ujuzi mkubwa. Katika Fasihi Simulizi wazee wa kitamaduni wanaweza kutumika kama wageni waalikwa. Mifano yao hasa katika jamii ambamo utafiti huu ulifanywa ni kama wazee walioendesha shughuli maalumu za matambiko na maapizo kama *Mangulieche* (Wanjala, 2013). Pia, shughuli za tohara (*khuminya na khulicha*) huendeshwa na wazee walio na tajiriba ya hali ya juu na ambao huzifahamu mila na desturi za jamii. Hawa aghalabu huyafahamu mambo mengi ya kale kwa undani sana. Mchango wao huwa mwafaka kabisa. Wageni hawa huweza kualikwa shuleni ama wanafunzi kuwatembelea katika maskani yao iwapo shule ina uwezo wa kifedha na kiusafiri. Wanapotumiwa, wanafunzi hufaidika sana. Walimu walioitumia mbinu hii walikiri kuwa wanafunzi wao waliichangamkia sana mbinu hii. Hata hivyo, inafaa pia itumiwe na mbinu zingine ili kusawazisha upungufu uwezao kutokea hasa wataalamu hao wakikosa kuimudu lugha ya Kiswahili barabara. Wajuzi hawa pia wanaweza kunaswa katika video na kisha kutumia tarakilishi kuhifadhi na katika matumizi yake ya baadaye.

#### 4.5.9 Kazi mradi

Walimu waliokiri kuitumia mbinu ya kazi mradi walikuwa sita (6) nao waliwakilisha asilimia sita (6%). Wanjala na Kavoi (k.h.j) wanasema kuwa kazi mradi ni mbinu ambayo wanafunzi hupatiwa kazi fulani na mwalimu kisha baadaye aiwasilishe darasani. Wanafunzi huelekezwa katika maktaba ama maeneo ya nyumbani ambako wanaweza kupata habari wazitakazo. Mbinu hii hutumiwa hasa wakati wa likizo ama mwisho wa juma ambapo muda wa kutosha hupatikana. Ubora wa mbinu hii ni kwamba wanafunzi huandaliwa kuwa watafiti mahiri wafikapo viwango vya juu vya kusoma kama vyuo vikuu. Walimu waitumiao mbinu hii huwanufaisha wanafunzi ingawa pia ni bora itumiwe pamoja na mbinu zingine ambazo ni za usasa kama tarakilishi na kinuruweo.

#### 4.5.10 Mbinu ya ziara

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (k.h.j) inafafanua ziara kama tendo la kwenda mahali fulani kwa sababu maalumu k.v. kutembelea au kufanya mazungumzo fulani. Mbinu hii ilichaguliwa na wasailiwa watatu (3) ama asilimia tatu (3%). Watumizi wa mbinu hii ya kufundishia Fasihi Simulizi ndio waliokuwa wachache kwa wote. Sababu iliyojitokeza ni kwamba mbinu hii ina gharama ya juu na huhitaji muda mwingi kwa ajili ya kufanya maandalizi. Aghalabu walimu huikwepa ili kupunguza gharama ya masomo. Hata hivyo, hii ni mbinu ambayo wanafunzi wengi huichangamkia sana kwani huwaondoa katika mazingira ya kufungiwa shuleni na darasani. Walimu waitumiao huwanufaisha wanafunzi kwa kiwango cha juu. Wanafunzi hunufaika iwapo mahali wanapotembelea ama magwiji wanaowahoji nyanjani watakuwa na tajiriba ya kutosha. Eneo mojawapo ambalo huwafaidi sana wanafunzi wa Fasihi Simulizi ni mapango ya *Kakapel* kule Teso ambako inaaminika ndiko tohara ya Wabukusu ilianzia. Pale ndipo shujaa wao, Mango, aliliua

joka na kisha kupashwa tohara kwa mara ya kwanza (Wanjala, k.h.j). Ili kufaulu katika kuitumia mbinu hii, itabidi kwamba walimu wajiandae vyema huku wakishirikiana na uongozi wa shule na walimu wengine ili kusafiri na kupata matokeo mema.

Jinsi tulivyoona katika mbinu zingine, ni muhimu kwamba mbinu hii itumiwe pamoja na mbinu zingine. Mbinu za kisasa kama tarakilishi zitachangamkiwa sana na wanafunzi kwa sababu ya usasa wake. Hali hii itawezesha ufunzaji bora wa wanafunzi hasa katika nyanja ya Fasihi Simulizi.

## 4.6 Hitimisho

Sura hii imechanganua data iliyokusanywa kulingana na malengo ya utafiti huu. Maelezo yametolewa kulingana na majibu ya wasailiwa katika hojaji, mahojiano na utazamaji. Matokeo haya yanaelekeza Mtafiti kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti katika sura ya tano.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti huu uliandaliwa kuchunguza matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi. Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Pia, sura inatoa mapendekezo kulingana na matokeo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa tasnifu

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo kulingana na malengo ya utafiti. Kazi yote ya utafiti ilipangwa kwa namna ifuatayo: Sura ya kwanza imeeleza kwa kina kuhusu mada ya utafiti. Sura hii imegawika katika sehemu tisa. Sehemu ya kwanza imeeleza utangulizi wa jumla wa mada ya utafiti. Sehemu ya pili imeeleza historia fupi ya ukuaji wa matumizi ya tarakilishi. Sehemu ya tatu imeeleza malengo ya utafiti. Sehemu ya nne imeeleza maswali ya utafiti. Sehemu ya tano imeeleza upeo na mipaka ya utafiti. Sehemu ya sita ikashughulikia sababu za kuchagua mada. Sehemu ya saba ilielezea umuhimu wa utafiti. Sehemu ya nane ikaangazia nadharia ya utafiti kisha sehemu ya mwisho imehitimisha sura hii.

Aidha, sura ya pili imeeleza baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu mbalimbali kuhusu matumizi ya tarakilishi. Sura imefafanua dhana ya tarakilishi, Fasihi Simulizi, matumizi ya vifaa vya kufunzia pamoja na matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia darasani. Nayo sura ya tatu imefafanua namna utafiti ulivyofanyika. Sura imegawanywa katika sehemu kumi ambazo ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la

utafiti na  kundi lengwa. Pia imeelezea sampuli ya utafiti na mchakato wa usampulishaji, mbinu za utafiti, uhalali na uthabiti wa mbinu hizo pamoja na uchanganuzi wa data. Halikadhalika maadili ya kitafiti yamefafanuliwa huku changamoto za utafiti zikielezwa..

Kadhalika, sura ya nne imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu. Nayo  sura ya tano ikitoa muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti. Sura hii imegawika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza imetoa muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili imefafanua matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sehemu ya tatu imeangazia mapendekezo yaliyotolewa na wasailiwa kuhusu namna ya kuimarisha matumizi ya tarakilishi shuleni. Sehemu ya mwisho imependekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti wa ziada.

### 5.2.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Utafiti huu uliochunguza " Matumizi ya tarakilishi katika kufunzia Fasihi Simulizi katika shule za upili nchini Kenya, mfano wa kaunti ya Bungoma." Utafiti ulifanyika  katika kaunti ya Bungoma nchini Kenya. Jumla ya wasailiwa hamsini na sita (56) walishiriki katika utafiti huu ambapo kumi na nane (18) walikuwa walimu wakuu na thelathini na sita (36) wakiwa walimu wa Kiswahili.

Utafiti ulikuwa na malengo manne makuu. Kwanza, kutathmini ni kwa kiwango kipi tarakilishi hutumiwa kama wenzo wa kufunza Fasihi Simulizi katika shule za upili katika kaunti ya Bungoma. Pili, kuchunguza jinsi walimu huandaa na kushirikisha tarakilishi wanapofunza Fasihi Simulizi katika shule za upili katika kaunti ya Bungoma. Tatu, kubainisha changamoto ambazo shule na walimu hukumbana nazo katika juhudi za kushirikisha tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi katika shule za upili katika

kaunti ya Bungoma. Kisha, kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa shule za upili za kaunti ya Bungoma katika kufundisha Fasihi Simulizi.

### 5.2.2 Viwango ambavyo walimu hutumia tarakilishi kufunzia Fasihi Simulizi

Mtafiti alipata kuwa shule zote zina tarakilishi lakini hutumiwa kwa shughuli za ofisi, kuchapisha mitihani, kufunza somo la tarakilishi, walimu kufanya utafiti na kuonyesha video za vitabu vya Fasihi. Walimu waliohojiwa walikiri kuwa wana ujuzi wa kutumia tarakilishi nao hutumia vifaa hivyo kwa shughuli za kibinafsi kama mawasiliano na utafiti lakini hawakuzitumia darasani kama wenzo wa kufunzia. Baadhi ya walimu pia walikubali kuwa wao hutumia tarakilishi kuonyesha kanda za vitabu vya Fasihi.

Mtafiti alithibitisha kuwa walimu wa Kiswahili hawatumii tarakilishi kufunza kipengee cha Fasihi Simulizi. Badala yake walimu hawa walitumia nyenzo zingine kama vifaa halisi, vitabu, fanani, michoro na chati.

### 5.2.3 Tarakilishi katika maandalizi na ufunzaji wa Fasihi Simulizi

Baada ya kuangalia maandalizi ya vipindi vya Fasihi Simulizi, Mtafiti alipata kuwa tarakilishi zilihusishwa kwa uchache katika vipindi hivyo vya Fasihi Simulizi. Alitambua kwamba walimu wote thelathini na sita (36) walipuuza tarakilishi katika kuandaa maazimio ya kazi kiasi kwamba hawakuiorodhesha tarakilishi kama wenzo wa kufundishia. Pia, maandalio ya masomo hayakuhusisha tarakilishi. Isitoshe madarasa, wanafunzi na walimu wasaidizi hawakutayarishwa kwa ajili ya vipindi vya kufunza Fasihi Simulizi kwa kutumia tarakilishi. Baadhi ya walimu, asilimia kumi (10) tu, ndio waliohusisha tarakilishi katika kuandaa nukuu za masomo tazama Jedwali 4.2. Kazi yao

ilionekana kuwa nadhifu zaidi ya kazi zingine zilizoandaliwa kwa maandishi katika madaftari.

### 5.2.4 Changamoto za kutumia tarakilishi

Kutokana na utafiti ilidhihirika kuwa kuna changamoto kadhaa katika kutumia tarakilishi kufundishia Fasihi Simulizi katika shule za upili. Asilimia sabini na mbili (72) ya walimu walikosa ujuzi wa kina na mazoea ya kutumia tarakilishi kama wenzo wa kufunzia. Wao walitumia tarakilishi kwa shughuli zingine tofauti hasa za kibinafsi. Ingawa shule zote kumi na nane (18) zilipatikana kuwa na tarakikilishi lakini zilitumiwa kwa shughuli tofauti shuleni. Wanafunzi walikuwa wengi na shule kumi (10) tu ndizo zilizokuwa na projekta. Kwa hivyo, walimu walidai kutotumia tarakilishi kwa kuwa ule uchache wazo hukuwafaidi wale wanafunzi wengi. Pia, walimu walilalamikia muda mchache wa dakika arobaini (40) kwa kila kipindi ilhali kuna vipengele vingi vya Fasihi Simulizi vinavyofaa kushughulikiwa. Tatizo la umeme kukatika kila mara, tarakilishi za viwango vya chini na kuharibika kwazo kulichangia walimu kukwepa teknolojia hii ya tarakilishi.

Kwa upande mwingine, walimu wakuu ishirini na nne (24) ama asilimia sitini na saba (67%), walikiri kuwa fedha shuleni ni chache kuwawezesha kununua tarakilishi za kutosha na za viwango vya juu. Pia, walimu walieleza kuwa baadhi yao hawakutumia kabisa tarakilishi kufunzia kwa kukosa ujuzi au kujitia hamnazo huku wakidai hawakuwa na muda wa kutosha kuandaa vipindi kwa kutumia tarakilishi. Walimu wa umri wa juu pia walikwepa kutumia teknolojia mpya kwani walikuwa na fikra kuwa walikuwa na ujuzi wa kutosha kutumia mitindo ya zamani katika kufunza Fasihi Simulizi.

### 5.2.5 Mbinu wanazotumia walimu kufunzia Fasihi Simulizi

Mtafiti aligundua kuwa kuna mbinu kadha ambazo walimu wa kaunti ya Bungoma hutumia katika kufundishia Fasihi Simulizi. Mbinu hizi ni pamoja na maelezo, maswali na majibu, majadiliano, maigizo, mihadhara, wageni waalikwa, kazi mradi, kanda za video pamoja na mbinu ya ziara. Urahisi wa kuzitumia nyingi ya mbinu hizi ndio unaowafanya wengi wa walimu kutohamasika na kutochangamkia kwa haraka mbinu ya tarakilishi.

## 5.3 Hitimisho

Sura hii imetoa maoni ya mwisho kwa mujibu wa matokeo yaliyopatikana katika utafiti. Asilimia ndogo ya walimu hutumia tarakilishi katika kufunzia Fasihi Simulizi shuleni. Pia walimu wachache huzishirikisha tarakilishi wanapofanya matayarisho ya kufunza Fasihi Simulizi. Halikadhalika, ilibainika kuwepo kwa changamoto tele katika kushirikisha tarakilishi katika ufunzaji wa Fasihi Simulizi. Hatimaye, ilidhihirika kwamba walimu wa Fasihi Simulizi hutumia nyenzo mbadala katika kufundisha Fasihi Simulizi.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, Mtafiti anatoa mapendekezo mbalimbali. Kwanza, kuwa tarakilishi ni muhimu sana katika ufunzaji, serikali na wadau wengine katika sekta ya elimu watoe tarakilishi za kutosha kwa shule. Tarakilishi hizi zitatumiwa kwa shughuli za kufunza ili wanafunzi wapate manufaa ya wenzo huu. Pia, Wizara ya Elimu iharakishe kutoa mada za masomo tofauti katika mfumo wa dijitali ili zitumiwe kama mwongozo katika shule zote.

Mafunzo ya ualimu yatilie mkazo mfumo wa kidijitali kuwasilisha ujumbe ili walimu wanapofuzu wawe na ujuzi wa kutosha kutumia teknolojia za kisasa katika ufunzaji. Mazoezi ya matumizi pia yatiliwe maanani ili walimu wapate ukakamavu wa kutumia teknolojia hii.

Mfumo wa elimu una vipengele vingi vya kushughulikiwa. Ingekuwa bora kama vipengele hivi vingepunguzwa au kuongezwa muda ili walimu wapate nafasi nzuri na ya kutosha. Hali hii itawawezesha kujiandaa na hata kutumia mbinu tofauti kufunzia ikiwemo teknolojia ya kisasa kama tarakilishi.

Tarakilishi ichukuliwe kama wenzo muhimu wa kufundishia na sio tu kutumiwa kwa shughuli zingine kama mawasiliano au burudani. Wizara ya Elimu na serikali kwa jumla inafaa kusambaza ukweli huu ili walimu na wanafunzi watiwe motisha ya kuthamini tarakilishi kama wenzo wa kisasa wa kufundishia masomo shuleni. Wenzo huu huwezi kupuuzwa kwani ndio kama mtambo unaouendesha ulimwengu wa sasa. Kwa hivyo kila mmoja wetu na hasa walimu inabidi tuenende na mabadiliko ya wakati na kukumbatia teknolojia mpya ijapo katika mazingira yetu. Tukichelea tutabaki nyuma kimaendeleo.
Kwa hivyo ni muhimu kwamba serikali ilichunguze suala hili ili walimu wapatiwe mafunzo mahsusi na hasa yanayolenga masomo wanayoyafundisha hususan Fasihi Simulizi. Iwapo haya yatatimizwa basi walimu wa Kiswahili watafaulu kutumia tarakilishi kufunzia vipengele vya Fasihi Simulizi bila kutoa madai yasiyo na msingi.

Walimu wa Kiswahili na hasa wanaofundisha Fasihi Simulizi hawana budi watambue kwamba matumizi ya tarakilishi huweza kuokoa muda sana na hivyo basi kuwa kifaa chema cha kutumia darasani. Ni jukumu la walimu hawa ni kufanya mazoezi ya kutosha

ili wawe na tajiriba ya kutumia tarakilishi. Ni bora wahudhurie warsha na mafunzo mbalimbali yanayolenga matumizi ya tarakilishi darasani na hata katika ujumla wake. Labda wakati umetimia kwa Wizara ya Elimu kutambua umuhimu wa matumizi ya tarakilishi katika kufundishia ili iweke mikakati mwafaka ya kufaulisha juhudi hizi. Wizara inapotoa mwongozo rasmi, basi wadau wakiwemo walimu hawatakuwa na lingine ila kutii na kutenda ipaswavyo.

Litakuwa jambo mwafaka iwapo juhudi za kina zitaimarishwa ili kuwasaidia walimu kutumia wenzo huu wa kisasa wa kufundishia. Huenda kwa kufanya hivyo somo la Kiswahili likaboreshwa hata zaidi huku matokeo ya mitihani ya kitaifa yakiimarishwa.

**5.5 Mapendekezo kwa tafiti za baadaye**

Utafiti huu ulizingatia tu matumizi ya tarakilishi kufunza Fasihi Simulizi. Mtafiti anapendekeza utafiti mwingine kufanywa katika sehemu zifuatazo:

Matumizi ya tarakilishi kufunzia vipengele vingine vya lugha ya Kiswahili katika shule za upili. Maeneo yanayoweza kulengwa ni kama vile sarufi, ufahamu, ufupisho, Isimu jamii, Fasihi Andishi pamoja na insha.

Aidha utafiti unaweza kufanywa kuonyesha athari za matumizi ya tarakilishi kwa wanafunzi wa viwango mbali mbali. Kuna wale wanafunzi wa chekechea, wa shule za msingi pamoja na wa vyuo vya juu.

Isitoshe, ujuzi wa walimu katika matumizi ya tarakilishi darasani unastahili kutafitiwa. Hii huenda ndiyo sababu kuu ya kwa nini kuna matumizi haba ya tarakilishi katika madarasa mengi shuleni mwetu. Hiki ni kinyume na namna mabadiliko yalivyo mengi na

maenezi ya usasa wa teknolojia katika ulimwengu wa leo. Ni muhimu basi swala hili lichunguzwe ili pawepo na mtazamo mpya.

# MAREJELEO


Agufana, J. (2000). Availability and use of learning-teaching resources for oral literature in Kiswahili in selected secondary schools in Uasin Gishu District. Tasnifu isiyochapishwa, Moi University, Eldoret.

Ajeyi, R. J. (1984). The position of visual audio in Teaching and Learning in selected Nigerian School. Post Graduate Diploma, Nairobi University.

Akivaga, S. K. na Odaga, A. B. (1985). *Oral literature*. *A School Certificate Course*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Alifa, C. na Dumu, K. (2017). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Longhorn.

Alonso, F. (2005). An instructional model for web-based learning with a blended learning approach. *British Journal of Education and Technology. Vol. 36/2.* Uk. 217-235.

Arege, T. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Printwell Industries Ltd.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Bates, A. (2005). *Technology, e-learning and Distance Education*. London: Routledge.

Brown, K. (1986). *Taking Advantage of Media*. Boston: Routledge na Kogan.

Chesaina, C. (2007). *The Role and Significance of Oral Literature in Social and Psychological Development of Children*. Nairobi: University of Nairobi.

Derek, E. (2003). ICT definitions. http://derek.stockley.com.au/elearning-definitionhtme.

Enon, C. J. (1998). *Education Research and Measurement*. Department of Distance Education. Kampala: Makerere University Press.

Farrant, J. (1992). *Principles and Practices of Education*. Singapore: Longman Publishers.

Gagne, R. M. (1977). *The Conditions of Learning*. *Toleo la 2*. New York: Holt Richard and Winston.

Gay, R. (2000). *Educational Research Conference for Analysis and Application. (Toleo la 4).* New Jersey.

Geer, R, na Sweeny, T. (2012). Students' voices about learning with Technology. *Social Sciences. Juzuu la 8 (2)* 294 – 303.

Gulbahar, Y. (2007). Technology planning, a roadmap for successful technology integration in schools. *Computers and Education. Juzuu la 49(4)* 943-956.

Iacono, J., Brown, A. na Holtham, C. (2009). Research methods. An example of participant observation. Jarida la *Business Research Methods. Juzuu la 7 (1).*

Johnson, H. M. (2007). Dialogue and the construction of knowledge exploring students' perception of their learning Eurodl. Organisation.

Joyce, B. (1992). *Model of Teaching*. Toleo la 4. New Delhi: Private Ltd.

Kafu, P. A. (2000). *Challenges of Teacher Education in the 21st Century*: *The Kenyan Experience*. Eldoret: Moi University Press.

Kamau, S. N. (2009). Kiswahili, utandawazi na umoja wa Afrika. *Journal of Language Technology and Entrepreneurship. Juzuu la 1*.

Kenya Beareau of statistics. (2007). https://www.knbs.or.ke

Kenya Institute of Education. (2002). *Mtaala wa Kiswahili Nchini Kenya*. Juzuu la 5.

Kenya National Examinations Council. (2007). Report, regulations and syllabi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kenya National Examination Council. (2014). *The Year 2013 Examination Report: Juzuu la 1.*

Kenya School Net. (2003). Preparing a workforce for the evolving information economy. *A Survey of ICT Access and Use in Kenyan Secondary Schools*. Nairobi: Summit strategies Ltd.

K.I.E. (2002). *Mtaala wa Kiswahili Nchini Kenya.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

King'ei, K. na Kisovi, C. N. (2003). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kothari, C. R. (2003). *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: New Age international Publishers Ltd.

Kress, T. M. (2008). *Critical praxis Research; Breathing New Life into Research Methods for Teachers*. United States of America: Springer.

Lickson, J. E. (2003). *Effects of Pictures on Anxiety and Text Learning*. New Jersey: Prentice Hall.

Maps.com. http://www.maphill.com/kenya/western/bungoma/`

Maranga, S. S. (1993). Su1ggestions of improving teaching-learning, administration and supervision in schools. Jarida la 3 (2) 240-245).

Matei, A. K. (2012). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.

Mbiti, D. M. na Ayot, H. O. (1984). *Language for Learning*. Nairobi: Macmillan Publishers.

Mrikaria, S. E. (2007). Fasihi Simulizi na teknolojia mpya. *Swahili Forum Juzuu la 14 (2)* 197-206.

Msokile, M. (1993). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es salaam: EPD.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (2003). *Social Science Research*. Nairobi. Act Press.

Muindi, A. (2008). *Changing the Kenyan Literary Landscape*. Nairobi: Ekitabu Publishers.

Mukwa, C. W. (1979). A field survey of tools and techniques for learning in secondary school education in Kenya. Tasnifu ya uzamifu. Michigan University.

Murray, K. na Waller, A. (2007). Social networking goes abroad. *Education Abroad. Juzuu la 16 (3);* 56-59.

Musau, P. M. (1999). Constraints on the planning and acquisition of indigenous languages. *The Case of Kiswahili in Kenya, Journal of Language and Culture. Juzuu la 12 (2)* 117-127.

Ibrahim, H. (1973). *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nandwa, J. na Bukenya, A. (1984). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman Kenya.

Njogu, K. (2006). *Fasihi Simulizi na Nadharia za Fasihi*. Nairobi: Twaweza Publications.

Nsubuga, E. H. K. (2000). *Fundamentals of Education Research*. Kampala: M. K. Publishers (U) Ltd.

Odeo, I. (2003). Matatizo ya kufundisha Fasihi Simulizi katika shule za sekondari. Makala katika *konganamo la CHAKITA.*

Oduro, P. (2008). A survey of instructional practices of teaching Kiswahili in upper primary schools in Nakuru district. Tasnifu ya uzamifu isiyochapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Orodho, A. J. (2003). *Essentials of Education and Social Sciences Research Methods.* Nairobi: Masola Publishers.

Oso, Y. W. na Onen, D. (2005). *A General Guide to Writing Research Proposal and Report.* Toleo la 2. Kampala: Makerere University Printery.

Republic of Kenya. (2007). *National ICT Strategy for Education and Training.* Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya. (2010). *Katiba ya Jamhuri ya Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Robertson, B. (2000). Using Distance Education and ICT to improve access, equity and equality in nivalareas.http://www.irodl.or.index.php.htme.

Rogers, E. M. (2003). *Diffusion of Innovations*. *Toleo la 5.* New York. Free Press.

Rotumoi, J. K. (2006). Availability and use of instructional media resources for the novel in selected secondary schools in Baringo county. Tasnifu ya Uzamili isiyochapishwa. Chuo Kikuu cha Moi.

Rubin, H. J. na Rubin I. S. (1995). *Qualitative Interviewing: The Art of Data Hearing*. London: Sage Publiations.

Singleton, A. R. (1993). *Approaches to Social Research*. Oxford University Press. New York.

Song, H. D. na Kang, T. (2012). Evaluating the impacts of ICT use in China. The Turkish on-line. Jarida la *Education Technology*. Imedondolewa kutoka http://academia.edu/1410234/.

Suter, E. na Busienei, A. J. (2013). Material and instructional approaches used by secondary school teachers of Kiswahili oral literature in Marakwet district, Kenya.

Tahir, G. (2002). Educating disadvantaged groups. The case of nomads in Nigeria. Jarida la *The World Council for Curriculum and Instruction 3(2)* 135-147.

Too, J. K. (1996). A Survey of the availability and use of media resources in Mathematics instruction in secondary schools in Nandi district, Kenya. Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi.

Tucker, R. (2007). Southern drift: The styles of first and third year students of the build environment. *Architectural Science Review, 50 (3),* 246 -255.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Volman, M. (2005). Variety of roles for a new type of teacher. *Education Technology and the Teacher 21* 15-31.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publication Limited.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.

Wanjala, F. S. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wanjala, F. S. na Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wanjala, M., Khaemba, E. na Mukwa, C. (2011). Significant factors in professional staff development for the implementation of ICT education in secondary schools: A case of schools in Bungoma District. *International Journal of Curriculum Instruction.*

Wanjuki, C. N. (2000). Factors affecting availability acquisition and utilisation of resources in the teaching of English in selected Kenyan secondary schools. Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Watson, D. M. (2001). Pedagogy before technology. *Rethinking the Relationship between ICT and Teaching Education and Information Technology 6-4*, 251-266.

Wasiche, F. A. (2009). Use of instructional media in teaching oral literature in Kiswahili in secondary schools in Bungoma district. Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi.

Wetende, C. M. (2015). Utilisation of educational media in teaching and learning of oral literature in Butere sub-county secondary schools, Kenya.

Wins, P. na Lawler, M. (2007). Investing in educational institutions in developing countries; An evaluation of their impact in Kenya. *Jarida la Kimataifa la Education. Juzuu la 6 (2)* 221 – 228.

Young, M. na Quinn, l. F. (2003). Heading the way, changing thinking from inputs to outputs htt://www.ci.unlu.ed/dpt/presentations/2003html.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Hojaji ya walimu wa Kiswahili

1. Jinsia Kike [ ] Kiume [ ]
2. Umri Miaka 20 – 30 [ ] 31 – 40 [ ] 41- 50 [ ] Zaidi ya 50 [ ]
3. Masomo
   - Shahada ya pili au zaidi [ ]
   - Shahada ya kwanza [ ]
   - Diploma [ ]
   - Cheti kingine [ ]
4. Ujuzi wa kufunza
   - Chini ya miaka 5 [ ]
   - Miaka 10 – 20 [ ]
   - Zaidi ya miaka 20 [ ]
5. Vipindi
   - 10 – 15 [ ]
   - 16 – 20 [ ]
   - 21 – 25 [ ]
   - 26 – 30 [ ]
6. a) Una ujuzi wowote kuhusu matumizi ya tarakilishi?

   ……………………………………………………………………………………

   b) Ulipataje ujuzi huo?

   7. a) Je, shule yako iko na tarakilishi?………………………………………

b) Ikiwa zipo, hutumiwa kufanya nini?

…………………………………………………………………………………………

8 a) Wewe binafsi umewahi kutumia tarakilishi hapa shuleni?

…………………………………………………………………………………………

b) Je, uliitumia kufanya nini?

…………………………………………………………………………………………

9 a) Je, umewai kutumia tarakilishi kufunza somo la Kiswahili?

…………………………………………………………………………………………

b) Ni kipengee kipi ulichofunza hasa?

…………………………………………………………………………………………

c) Maandalizi ya kipindi hiki yalihusisha nini hasa?

………………………………………………………………………………………… ……

d) Je, uliweza kuafikia lengo lako katika hicho kipindi ulichotumia tarakilishi kufunza?.......................................................................................................................

e) Taja baadhi ya changamoto ambazo umekumbana nazo katika matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia.


……………………………………………………………………………………………

f) Toa maoni yako binafsi (kwa ufupi) kuhusu tarakilishi kama kifaa cha kufunzia.

……………………………………………………………………………………………

10. Mbali na tarakilishi, wewe kama mwalimu hutumia mbinu zipi katika kufundishia Fasihi Simulizi?.......................................................................................................

## Kiambatisho 2: Hojaji ya walimu (Mfano wa nakala iliyojazwa)



√ 16
① √

HOJAJI YA WALIMU

1. Jinsia Kike [✓] Kiume [ ]
2. Umri Miaka 20 – 30 [ ] 31 – 40 [ ] 41- 50 [ ✓ ]
   Zaidi ya 50 [ ]
3. Masomo
   - Shahada ya pili au zaidi [ ]
   - Shahada ya kwanza [✓]
   - Diploma [ ]
   - Cheti kingine [ ]
4. Ujuzi wa kufunza
   - Chini ya miaka 5 [✓]
   - Miaka 10 – 20 [ ]
   - Zaidi ya miaka 20 [ ]
5. Vipindi
   - 10 – 15 [ ]
   - 16 – 20 [ ]
   - 21 – 25 [✓]
   - 26 – 30 [ ]

6 a) Una ujuzi wowote kuhusu matumizi ya tarakilishi?
.........ndiyo.........

b) Ulipataje ujuzi huo?
.........mafunzo yaliandaliwa shuleni.........

7 a) Je, shule yako iko na tarakilishi?
.........ndiyo.........

b) Ikiwa zipo, hutumiwa kufanya nini?
.........kazi za ofisi, mitihani.........

8 a) Wewe binafsi umewahi kutumia tarakilishi hapa shuleni?
ndiyo.

30

……………………………………………………………………………………………

b) Je, uliitumia kufanya nini?

majaribio wakati wa kufundishwa hapa shuleni.

9 a) Je, umewai kutumia tarakilishi kufunza somo la Kiswahili?

ndiyo

b) Ni kipengee kipi ulichofunza hasa?

kuonyesha video za vitabu vya fasihi.

c) Maandalizi ya kipindi hiki yalihusisha nini hasa?

kutafuta kanda na kuwaonyesha wanafunzi.

d) Je, uliweza kuafikia lengo lako katika hicho kipindi ulichotumia tarakilishi kufunza?

ndiyo, wanafunzi kujadili vile vitabu kwa urahisi.

10. Taja baadhi ya changamoto ambazo umekumbana nazo katika matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia.

- tarakilishi chache.
- umeme kupotea wakati wa maonyesho.
- kungekuwa na projekta.

11. Toa maoni yako binafsi (kwa ufupi) kuhusu tarakilishi kama kifaa cha kufunzia.

- Ni kifaa bora.
- wanafunzi wanafurahia matumizi yake.
- kubadili njia za kufunza

**Kiambatisho 3: Mahojiano na walimu**

1. Kiwango chako cha elimu ni kipi?

…………………………………………………………………………………………

2. Umefundisha Kiswahili kwa muda gani?

…………………………………………………………………………………………

3. Wewe hufunza vipindi vingapi kwa jumla?

…………………………………………………………………………………………

4. Una ujuzi wowote kuhusu matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji?

…………………………………………………………………………………………

5. Katika shule yako kuna tarakilishi?

………………………………………………………………………………………..

6. Wewe umewahi kutumia tarakilishi kufundisha somo la Kiswahili?

………………………………………………………………………………………..

7. Ni kipengele kipi ulichofunza?

……………………………………………………………………………………………

8. Ulijiandaa vipi kwa kipindi hicho? Fafanua kifupi.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………….............

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

9. Kulingana na wewe, wanafunzi walichukulia vipi kipindi hicho?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

10. Je, una maoni yapi kuhusu tarakilishi kama mojawapo ya vifaa vya kufunzia na hasa somo la Fasihi Simulizi?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

11. Ni mbinu zipi zingine unazozitumia katika kufundishia Fasihi Simulizi?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**Kiambatisho 4: Mahojiano na walimu (Mfano wa nakala iliyojazwa)**

MAHOJIANO NA WALIMU

1. Kiwango chako cha elimu ni kipi? Shahada ya kwanza
2. Umefundisha Kiswahili kwa muda gani? – Miaka 5
3. Wewe hufunza vipindi vingapi kwa juma? — 22
4. Una ujuzi wowote kuhusu matumizi ya tarakilishi katika ufunzaji? Ndiyo
5. Katika shule yako kuna tarakilishi? — ndiyo
6. Wewe umewahi kutumia tarakilishi kufundisha somo la Kiswahili? – Ndiyo
7. Ni kipengele kipi ulichofunza ? — Fasihi Andishi (vitabu)
8. Ulijiandaa vipi kwa kipindi hicho? Fafanua kidogo.
9. Kulingana na wewe, wanafunzi walichukulia vipi kipindi hicho?
10. Je, una maoni yapi kuhusu tarakilishi kama mojawapo ya vifaa vya kufunzia na hasa somo la fasihi simulizi?

8 – Kutafuta kanda zilizo na uigizaji wa vitabu vya fasihi.
– Kuweka wanafunzi mahali maalum na kuwaonyesha kanda kupitia televisheni.

9. Walifurahia yale maonyesho ya uigizaji.

10. Kifaa hiki ni bora. ~~Kinafaa~~ kuwatulizi- mwa darasa.

32

**Kiambatisho 5: Hojaji ya walimu wakuu**

1. Idadi ya wanafunzi

   200 – 500 [ ] 500 – 1000 [ ]

   Zaidi ya 1000 [ ]

2. Idadi ya walimu

   Chini ya 20 [ ] 20 – 50 [ ]

   Zaidi ya 50 [ ]

3. Una ujuzi wowote kuhusu matumizi ya tarakilishi?

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

4. Shule yako ina tarakilishi?

   ………………………………………………………………………………………

5. Taja baadhi ya kazi za tarakilishi katika shule yako?

   …………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………

6. Ni walimu wangapi katika shule yako walio na ujuzi wa kutumia tarakilishi?

   ………………………………………………………………………………………

7. Je, walimu hawa hutumia tarakilishi kufunzia darasani?

   ………………………………………………………………………………………

8. Walimu wako wamewahi kuhudhuria mafunzo ya matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia?

   ……………………………………………………………………………………..

9. Shule yako imeandaa warsha yoyote kufunza walimu matumizi ya tarakilishi darasani?

……………………………………………………………………………………….

10. Wewe hupata vipi vifaa vya kufunzia na hasa tarakilishi?

……………………………………………………………………………………….

11. Shule yako ina mpango gani kuhakikisha walimu wanatumia teknolojia  za kisasa kufunza na hasa tarakilishi?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

12. Ni changamoto zipi unakumbana nazo katika matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

13. Kwa ufupi toa maoni yako binafsi kuhusu tarakilishi kama kifaa cha kufunzia?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

## Kiambatisho 6: Hojaji ya walimu wakuu (Mfano wa nakala iliyojazwa)

### HOJAJI YA MWALIMU MKUU

1. Idadi ya wanafunzi

   200 -- 500 [✓] 500 – 1000 [ ]
   Zaidi ya 1000 [ ]

2. Idadi ya walimu

   Chini ya 20 [✓] 20 – 50 [ ]
   Zaidi ya 50 [ ]

3. Una ujuzi wowote kuhusu matumizi ya tarakilishi?

   ........Ndiyo..........................................................................

4. Shule yako ina tarakilishi?

   ........Ndiyo..........................................................................

5. Taja baadhi ya kazi za tarakilishi katika shule yako?

   ........Shughuli za kiofisi..............................................................
   ........Kuchapisha mitihani..........................................................

6. Ni walimu wangapi katika shule yako walio na ujuzi wa kutumia tarakilishi?

   ........Wote (20)........................

7. Je, walimu hawa hutumia tarakilishi kufunzia darasani?

   ........La.................................................................

8. Walimu wako wamewahi kuhudhuria mafunzo ya matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia?

   ........Wachache..........................................................................

9. Shule yako imeandaa warsha yoyote kufunza walimu matumizi ya tarakilishi darasani?

   ........La.....................................................

10. Wewe hupata vipi vifaa vya kufunzia na hasa tarakilishi?

    ...Ufadhili wa serikali.......................................
    Wadhamini

33

11. Shule yako ina mpango gani kuhakikisha walimu wanatumia teknolojia za kisasa kufunza na hasa tarakilishi?

....Kuwapa mafunzo kuhusu umuhimu wa....

....tarakilishi kufunza....

12. Ni changamoto zipi unakumbana nazo katika matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufunzia?

....Walimu kutopendelea kutumia....

........................................................................................

13. Kwa ufupi toa maoni yako binafsi kuhusu tarakilishi kama kifaa cha kufunzia?

....Ni kifaa kinachofaa sana....

........................................................................................

........................................................................................

**Kiambatisho 7: Utazamaji wa kipindi**

1. Tarehe:…………………………………………………………………………………
2. Shule yako ni ya jinsia gani?

   Wavulana [ ] Wasichana [ ] Mseto [ ]
3. Kuwepo kwa vifaa vya umeme…………………………………………………..
4. Kuwepo kwa tarakilishi shuleni…………………………………………………..
5. Je, mwalimu amehusisha tarakilishi kama kifaa cha kufunzia katika maandalizi ya somo lake ?.........................................................................................
7. Ni wakati upi tarakilishi inatumiwa katika kipindi?...............................................
8. Ni vipi mwalimu ametumia tarakilishi katika kipindi chake? ...............................................................................................................................

   ..............................................................................................................................
9. Je,wanafunzi wanaonyesha athari yoyote tarakilishi inapotumiwa katika somo? Fafanua kidogo.

   …………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………….
10. Tathmini ujuzi wa mwalimu katika kutumia tarakilishi kufunza somo la Fasihi Simulizi.

    …………………………………………………………………………………………

    …………………………………………………………………………………………

**Kiambatisho 8: Utazamaji wa kipindi (Mfano wa nakala iliyojazwa)**

**KIAMBATISHO 7: UTAZAMAJI WA KIPINDI**

1. Tarehe: 19/6/2017

2. Shule yako ni ya jinsia gani?

   Wavulana [ ] Wasichana [✓] Mseto [ ]

3. Kuwepo kwa vifaa vya umeme Kuna Stima

4. Kuwepo kwa tarakilishi shuleni Zipo chache

5. Je, mwalimu amehusisha tarakilishi kama kifaa cha kufunzia katika maandalizi ya somo lake ? La.

6. Ni wakati upi tarakilishi inatumiwa katika kipindi? hakutumia

7. Ni vipi mwalimu ametumia tarakilishi katika kipindi chake?

   hakutumia.

8. Je,wanafunzi wanaonyesha athari yoyote tarakilishi inapotumiwa katika somo? Fafanua kidogo.

   Wanafunzi hawakuthathminiwa.

9. Tathmini ujuzi wa mwalimu katika kutumia tarakilishi kufunza somo la Fasihi Simulizi.

   Mwalimu hakutumia tarakilishi kwa hivyo hangethathminiwa.

**Kiambatisho 9: Mfano wa azimio la kazi**

**ST. AUGUSTINE GIRLS LUKHUNA**

**AZIMIO LA KAZI, KIDATO CHA PILI, MUHULA WA PILI; 2017**

**ASILIA:** KLB, Mwongozo wa Mwalimu, Kitabu cha Mwanafunzi, Kamusi, CHEMCHEMI, Mwongozowa Mwalimu, Kitabu cha Mwanafunzi.

| JMA | KPN | SOMO | SHABAHA | MBINU | VIFAA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 4-6 | **KUFUNGUA NA KUSAHIHISHA KAZI YA LIKIZO** | | | |
| 2 | 1 | Sarufi<br>Uakifishaji | **Kufika mwisho wa funzo mwanafunzi aweze;**<br>Kubainisha alama mbalimbali za uakifishaji | Kutambua<br>Kuandika | Chaki<br>Ubao<br>Madaftari |
| | 2 | Kuandika<br>Barua rasmi | **Kufika mwisho wa funzo mwanafunzi aweze;**<br>Kuandika mtungo wenye mantiki | Kuandika | Chaki<br>Ubao<br>Madaftari |
| | | Kusoma<br>Ufahamu | **Kufika mwisho wa funzo mwanafunzi aweze;**<br>Kujibu maswali ya ufahamu | Kusoma<br>Kujadili<br>Kuandika | Chaki<br>Ubao<br>Madaftari |
| | 4 | Kuandika<br>Maelezo/maagizo | **Kufika mwisho wa funzo mwanafunzi aweze;**<br>Kuandika hati nadhifu | Kuandika | Chaki<br>Ubao<br>Madaftari |
| | 5 | Fasihi | **Kufika mwisho wa funzo** | | Chaki |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hekaya | **mwanafunzi aweze;**<br><br>Kuchambua hadithi aliyopewa | Kusoma<br><br>Kuandika | Ubao<br><br>Madaftari |
| 3 | 1 | Kusoma<br><br>Muhtasari | **Kufika mwisho wa funzo mwanafunzi aweze;**<br><br>Kufupisha makala bila kupoteza maana | Kusoma<br><br>Kufupisha | Chaki<br><br>Ubao<br><br>Madaftari |
| | 2 | Sarufi<br><br>Usemi halisi | **Kufika mwisho wa funzo mwanafunzi aweze;**<br><br>Kutumia usemi halisi katika sentensi | Kutambua<br><br>Kutunga sentensi<br><br>Kufanya zoezi | Chaki<br><br>Ubao<br><br>Madaftari |

**Kiambatisho 10: Mbinu za kufundishia miongoni mwa walimu**

| Mbinu za kufundishia | Walimu waliotumia | Asilimia |
|---|---|---|
| Maelezo | 20 | 20 |
| Maswali na majibu | 25 | 24 |
| Majadiliano | 18 | 17 |
| Maigizo | 06 | 6 |
| Mhadhara | 04 | 4 |
| Wageni waalikwa | 05 | 5 |
| Kazi mradi | 06 | 6 |
| Kanda video | 15 | 15 |
| Ziara za nyanjani | 03 | 3 |
| **JUMLA** | **102** | **100** |

**Kiambatisho 11: Ramani ya kaunti ya Bungoma**




http://www.maphill.com/kenya/western/bungoma/sirisia/

## Kiambatisho 12: Barua ya idhini kutoka SGS

**KIBABII UNIVERSITY**
*(Knowledge for Development)*

Tel: 020 – 2028660 / 0708 – 085934 / 0734 - 831729
P.O. Box 1699 – 50200
Bungoma
Kenya

E-mail: enquiries@kibabiiuniversity.ac.ke /
registrar.adm58@yahoo.com
Website: http://www.kibabiiuniversity.ac.ke

**Ref**: KIBU/SGS/CORR.033/VOL.1-2014/077

**Date:** 26th September, 2017

**Dear:** Kibiti David Barasa
**Reg No:** MED/KIS/006/14

**RE: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

I am pleased to inform you that the Senate of Kibabii University acting on the advice of the Board of the School of Graduate Studies approved your proposal Entitled: **"Matumizi ya Tarakilishi katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi Katika Shule za Kenya."** and appointed the following as supervisors:

1. Dr. Wanjala Fred Simiyu
2. Dr. Ben Nyongesa

You will be required to submit through your supervisor(s) progress reports every three months to the Dean SGS. Reports should be copied to the following: Chairman, FGSC-FESS and Chairman, DGSC-KOAL

It is the policy of the University that you observe a deadline of Two years from the date of registration for a Masters thesis. Do not hesitate to consult this office incase of any problem encountered in the course of your work.

Yours Sincerely,

Prof S. N. Mutsotso
**Dean, SGS**

**Copy to:** Vice Chancellor
DVC(ASA)
DVC ( AFD)
DVC ( PPRI)
Director PC & QA

**Kibabii University ISO 9001:2008 Certified**
**Knowledge for Development**

Page 1 of 1

*PSNM/pi*

## Kiambatisho 13: Barua ya idhini kutoka NACOSTI

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. KIBITI DAVID BARASA***
**of KIBABII UNIVERSITY, 377-50200**
**Bungoma,has been permitted to**
**conduct research in *Bungoma County***

**Permit No : NACOSTI/P/17/80954/19449**
**Date Of Issue : 13th October,2017**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



**on the topic: *MATUMIZI YA TARAKILISHI KATIKA KUFUNDISHIA FASIHI SIMULIZI***

**for the period ending:**
***12th October,2018***

.............................
***Applicant's Signature***

...............................................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

# CONDITIONS

1. The License is valid for the proposed research, research site specified period.
2. Both the Licence and any rights thereunder are non-transferable.
3. Upon request of the Commission, the Licensee shall submit a progress report.
4. The Licensee shall report to the County Director of Education and County Governor in the area of research before commencement of the research.
5. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further permissions from relevant Government agencies.
6. This Licence does not give authority to transfer research materials.
7. The Licensee shall submit two (2) hard copies and upload a soft copy of their final report.
8. The Commission reserves the right to modify the conditions of this Licence including its cancellation without prior notice.

Science, Technology and Innovation National Commission for Science, Technology